# *El-Shaddai*

Asante, ndugu.

2 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Ni wangapi wangetaka kukumbukwa, usiku wa leo, katika maombi kwa kuinua tu mikono yenu, tafadhalini? Asanteni.

3 Baba wa Mbinguni mwenye rehema, usiku wa leo tunashukuru ya kwamba tunasimama katika kivuli cha rehema Yako, nasi tunaomba ya kwamba tutapewa hizo rehema za Kiungu. Tuna furaha sana kwamba Yesu alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi, na sasa ametuleta karibu na Mungu kwa kumwaga Damu Yake ili tuweze kusamehewa dhambi zetu, na—na kuwa na haki kwa ule Mti wa Uzima.

4 Na usiku wa leo, tunapoangalia kote mle ndani, kwenye chumba cha dharura na kuwaona hao watu wa thamani wakiwa wagonjwa sana, na karibu kufa, na kuhisi nguvu hizo za Kiungu za Mungu zikiingia, kama mawimbi juu ya hi—hili jengo, tunajua, Baba, ya kwamba Wewe uko karibu kuwapa rehema wote watakaokuita na kuamini.

5 Kuna wengi wanaoketi hapa ndani usiku wa leo, Bwana, katika vivuli vya mauti, jalia, ibada hii itakapokwisha, mauti na yaondoke, tujalie, Bwana, na jalia uhai wa Mungu uingie, uwape maisha mapya, na matumaini mapya, afya mpya kwa wale walio wagonjwa na wanaoteseka. Kwa wale wasio na Mungu, na wasio na Kristo ulimwenguni, wametengwa, jalia Nuru kuu iangaze njiani mwao usiku wa leo, jalia wawe wanafunzi Wako.

6 Tusamehe jambo lolote ambalo tumefanya au kusema ambalo lingezuia maombi haya kujibiwa. Na jalia Roho Mtakatifu ashike hatamu za mkutano na kuitahiri mioyo yetu kutoka kutokuamini hadi imani katika Mungu, ili Mungu aweze kutenda kazi kupitia kwetu usiku wa leo, kufanya mapenzi Yake maishani mwetu, na kwa ajili ya wengine. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

7 Ketini. Ni majaliwa makubwa sana kuja na kuwaombea watu. Mara nyingi hilo, kama nilivyokuwa nikisema kwenye chumba cha dharura muda mfupi tu uliopita kwa baadhi ya watu wa thamani sana wapate kuombewa, "Ishara haziponyi." Mnaona? Hilo lilikuwa tu ni thibitisho la agizo la—langu la kuwaombea wagonjwa. Ono halingemponya mtu yeyote, wala ishara nyingine yoyote isingemponya mtu yeyote. Lakini ni—ni ninii, thibitisho la agizo, wakati alipozungumza nami usiku huo miaka kumi na minne iliyopita, tarehe saba Mei, Akasema, "Ulizaliwa kuwaombea wagonjwa," na akaniambia niende kote ulimwenguni.

Nami nikamwambia, "Hawataniamini, kwa sababu sina elimu, nami . . ."

8 Naye akasema kama vile Musa alivyopewa ishara mbili, ya kwamba nitapewa ishara mbili. Alisema ya kwanza, watu wangeweka mikono yao juu ya wangu, na ndipo ningeweza, kama sitatumia akili yangu mwenyewe, ku—kuwaambia tu shida yao, Yeye angeisema. Kisha kasema, "Kama utakuwa mwaminifu, itakuwa kwamba utajua siri yenyewe ya moyo wao."

9 Nanyi nyote mnajua hadithi hiyo, na mumekisoma kitabu hicho. Hilo ndilo lililonipeleka huko. Wengi wa ndugu zangu wameniambia hilo lilikuwa ni la ibilisi. Sasa, ninampenda Bwana Yesu, sikutaka chochote cha ibilisi, na kwa hiyo nilikuwa pale kukaa mpaka hilo liniache. Na ndipo aliponiambia kuhusu Maandiko, ndipo nikajua alikuwa sahihi; hiki Kitabu kilikuwa kipya kwangu.

Naye akasema, ya kwamba, kwa hilo wangeamini.

10 Sasa mnaona, hilo si . . . Kwa sababu kile ninachopungukiwa kwa kuwa mhubiri, kuwa na elimu, nilipewa hii kulipia hiyo. Ambapo mtu mwenye elimu nzuri, ya kiakili, na anajua angeweza, na anakijua hiki Kitabu vizuri sana, na alielimika, angeweza kukielezea hivi kwamba, aliitwa kuwa m—mhubiri, kama walioketi hapa pamoja nami usiku wa leo. Wahubiri wazuri, na wainjilisti, na wachungaji, wameitiwa hilo, vema, mahali nimepungukiwa na hiyo, hii nyingine inachukua mahali pake. Lakini nilipaswa kuninii, kuwaombea wagonjwa. Na maombi ndiyo yanayobadilisha mambo, mnaona.

11 Hivi mnajua maombi yanaweza kubadilisha nia ya Mungu? Mlijua hilo? Huyabadilisha, naam. Ninakumbuka wakati mmoja katika Biblia yalifanya hivyo. Mnakumbuka?

12 Tulikuwa na maskini kiamshakinywa kizuri kuliko vyote asubuhi hii nilichopata kuwa nacho, maishani mwangu mwote. Ni wakati mzuri jinsi gani tuliokuwa nao kwenye ushirika wa wachungaji hawa hapa! Naye Ndugu Hobson hapa, alitoa tamshi kwamba, kama sitaendelea na Ibrahimu usiku wa leo, ningependa kutoa baadhi ya—ya yaliyomo kutoka kwake. Alitusimulia hadithi hiyo, ambayo ilikuwa ya kusisimua sana ya watu watatu waliokuwa hotelini, ama mahali ambapo wa—waliacha ninii yao . . . Lifti iliharibika, ikawabidi kupanda vipandio sabini kwa miguu.

13 Walikubaliana ya kwamba kupanda juu hivi wangeninii, kila mmoja angesimulia jinsi ambavyo, tukio fulani la maisha. Hadithi ishirini, mmoja alisimulia, na hadithi hamsini, sitini, huyo mwingine alisimulia tukio lake, na juu kabisa huyo jamaa akasema, "Vema, lile tukio kuu, ambalo nimekuwa nalo, moja la kipekee sana ni sasa hivi, niliacha funguo zangu kwenye dawati."

14 Nashangaa tu kama mara nyingi katika matukio yetu ya Kipentekoste ya kujaribu kujenga kanisa kubwa, ama kufanya

jambo fulani kuwaingiza watu wengi sana, kama hatuachi ufunguo, mambo ya kimbinguni, kile hasa tunachotetea, Pentekoste, kama hatuuachi kwenye dawati. Kama ndivyo, hebu na tushuke kwenye vipandio haraka sana usiku wa leo, na kuuchukua, ili tuweze kuufungua mlango, maana haingeleta tofauti kubwa kwamba tulipanda juu kiasi gani, maadamu hatukuwa na kitu cha kuingilia baada ya kufika huko.

Hilo lilikuwa zuri sana, ndugu, bila shaka nililithamini hilo.

15 Ushirika mzuri sana tuliokuwa nao asubuhi ya leo, nami hakika nina furaha kujua ya kwamba Yakima ina kundi zuri la wachungaji hapa. Mungu. . .Wasikilizeni, ndugu na dada, wasikilizeni, watawaambia njia ya Uzima.

16 Sasa, sikuzote mimi huchelewa. Mimi, Mama alisema nilizaliwa nimechelewa kidogo, na sikuzote shuleni nilichelewa, kadi yangu ya ripoti ilikuwa, "Mchelewaji, mchelewaji, mchelewaji, mchelewaji," kote kote. Nilipofunga ndoa, pia nilikuwa nimechelewa, nilimfanya angoje kwa karibu saa moja na nusu, nami ilinilazimu kuwatembelea wagonjwa kwanza. Na kwa hiyo, kama ninaweza tu kuchelewa kwenye mazishi yangu, sasa, itakuwa sawa.

17 Nilikuja kwenye Kanisa la Evangelical United Brethren huko New Albany, Indiana, hivi majuzi, nami nilikuwa tu nimechelewa kwa yapata nusu saa, ndipo mchungaji akaamka, watu hao, walikuwa tayari kwenda nyumbani kufikia wakati huo, nao wakasema, mchungaji akasema, "Sasa ninatambulisha kwenu mchelewaji Bw. Branham." [Katika Kiingereza 'the late' inaweza pia ikawa na maana ya marehemu—Mfa.]

18 Vema, inanikumbusha juu ya, Ndugu Sweet, yuko hapa mahali fulani usiku wa leo, Ndugu Sweats, hasa, alikuwa hapa asubuhi ya leo mkutanoni. Tulikuwa huko Jamaika hivi majuzi, tukakutana huko Kingston, nilipokuwa kwenye uwanja wa mashindano ya farasi, naye alikuwa akiniimbia. Ndipo usiku huo, watu mashuhuri wa hicho kisiwa, walikuwa wametuleta nje kwa chakula cha mchana cha Wafanyabiashara, nao watu walikuwa huko kote kote kutoka Kuba kuhudhuria chakula hiki cha mchana, cha watengeneza viatu, wakuza miwa, na kadhalika. Na kwa hiyo jamaa mmoja akaniambia, akasema, "Je, wewe ni mhubiri?"

Nikasema, "Natumaini hivyo."

Akasema, "Una shughuli gani kuambatana na hawa Wafanyabiashara Wakristo?"

Nikasema, "Vema, mimi—mimi—mimi ni mfanyabiashara."

Kasema, "Loo, wewe ni mfanyabiashara?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Unafanya nini?"

Nikasema, "Mimi ni mwuzaji."

Akasema, "Unauza nini?"

Nikasema, "Hakikisho." *Hakikisho*, sio *bima*, *hakikisho*.

Akasema, "Ati nini," hakunielewa, akasema, "ni bima gani hiyo?"

Nikasema, "*Hakikisho Lililobarikiwa*."

Naye akasema, "Loo."

19 "Nauza hilo." Nikasema, "Kama mtu yeyote hapa usiku wa leo, anataka hati ya makataba, ningependa kuizungumzia pamoja nawe, hakika ningependa kuwaambia habari zake. Mimi, wakala wa Kampuni ya Bima ya Uzima wa Milele."

20 Kwa hiyo, ningetaka kuizungumzia na yeyote wenu hapa madhabahuni, nami nina hakika tunaweza, tuna baadhi ya mawakala hapa, wangeendeleza hiyo hati moja kwa moja na kuendelea, mnaona, wanaiendeleza.

21 Rafiki yangu mmoja, Wilmer Snyder, ana ndugu Mbaptisti hapa nje mahali fulani, anayehubiri, Courtney. Kama yupo hapa, ningetaka kukupa mikono tena, Court. Basi mimi na Wilmer tulikuwa marafiki wazuri sana shuleni, naye akasema, siku moja alianza kuuza bima, kwa hiyo akaja nyumbani kwangu, na akasema, "Billy, ningetaka kuzungumza nawe kuhusu bima."

22 Sasa, bima ni sawa, bali sina yoyote ya aina hiyo. Daima tunamlipa mtayarisha mazishi, kwa nini tusimpe kidogo *Mpeleka-Juu*, badala ya mzishi? Kwa hiyo—kwa hiyo mimi . . . Bima ni sawa, mnaelewa hilo. Sisemi lolote kuhusu . . .

Akasema, "Billy, ningetaka kuzungumza nawe kuhusu bima fulani."

Nami nikasema, "Loo, ninayo, Wilmer."

"Loo," akasema, "samahani."

"Ndugu yangu ni wakala wa bima."

Kwa hiyo akasema, "Loo, samahani," Kasema, "Nisingemwingilia Jesse, ndugu yako."

Nikasema, "La." Nikasema, "Nina hakikisho."

Naye akasema . . . Basi mke wangu akaniangalia nikisimama pale kana kwamba nilikuwa mnafiki. Mnaona? Akainua macho yake, akawaza, "Vema, ni kitu gani hiki?"

Naye akasema, "Uko na kampuni gani?"

Nikasema, "Uzima wa Milele."

Naye akasema, "Loo," akasema, "hilo ni zuri sana, Billy, lakini nitakwambia jambo fulani, hiyo haitakulaza makaburini huku nje."

Nikasema, "La, lakini itanitoa humo. Sina hamu ya kuingia humo," Nikasema, "Nina hamu ya kutoka humo."

23 Kwa hiyo, kama mtu yeyote anavutiwa na hati kama hiyo, wala hana moja, vema tungetaka. . .Hiyo ni kweli, ndugu? Sisi ni mawakala hapa wa hiyo usiku wa leo. Naam, bwana. Sihofu kuhusu kuingia makaburini, cha muhimu ni kutoka humo. Kwa hiyo, hilo ndilo ninalojaribu kusema, ni njia ya kutokea, na Kristo ndiye njia hiyo. Nami nina furaha sana ninalo hilo hakikisho.

24 Na papa hapa mbele zetu, kila mmoja wetu, umewekwa mlango mkubwa mno, mweusi, najua umewekwa mbele yangu, kila wakati moyo wangu unapopiga, niko pigo moja karibu zaidi na mlango huo, unaitwa mauti. Nami nitakapofika mahali hapo ambapo ninajua pigo langu la mwisho linapiga, nami sina budi kwenda mahali hapo, sitaki kwenda nikipiga mayowe kama mwoga, ninataka kujifunika kwa mavazi ya haki Yake, na kuingia kwenye mauti yangu, nikijua jambo hili: kwamba ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake, kwamba atakapoita, nitatoka miongoni mwa wafu siku moja. Na hilo ndilo kusudi letu la kuwa hapa.

25 Sasa, tunaninii. . .Nitajaribu kumalizia somo langu usiku wa leo la *Yehova-Yire* ikiwezekana. Tulichukuliwa tu *kabisa* jana usiku, ndani yake. Kwa hiyo, tulimwacha Ibrahimu, jana usiku, safarini kama mzee wa miaka sabini na mitano, ambaye Mungu alikuwa amemwita, na alikuwa ameitisha utengano mkamilifu. Nasi tulijifunza katika somo letu jana usiku ya kwamba Mungu anahitaji utengano mkamilifu na ulimwengu wote. Nayo Maandiko yanasema, “Ukiipenda dunia, ama mambo ya dunia,” hiyo ni kwa Uzao wa Ibrahimu, “kumpenda Mungu hakumo ndani yako.”

26 Kwa hiyo hatuna budi kufikia mahali katika Mungu, mahali fulani katika neema Yake, mpaka mambo na anasa za ulimwengu, si—simaanishi anasa za kimwili kama vile ungetoka na kuketi chini ya mti na kuburudika, ama kusafiri kidogo kwenye gari lako, lakini ninamaanisha anasa za *ulimwengu*, kunywa pombe, kucheza kamari, na mambo maovu, kama ungali unayapenda hayo, kumpenda Mungu hakumo ndani yako. Hivyo ndivyo tunavyoweza kujichunguza wenyewe kuona kama tunayo imani ama hatuna wakati mambo ya ulimwengu yamekufa na kutuondokea.

27 Ndipo basi Ibrahimu, tuliona, hakumtii Mungu ipasavyo. Sasa, alijiweka tayari na alikuwa na imani katika ile ahadi. Lakini mnaona, tungali tunaweza kuwa na imani katika ahadi halafu tusitii, ingali itatuzuia.

28 Sasa, unaweza kusema, “Nimeninii. . .Ni—ninamwamini Roho Mtakatifu, ninaamini ninapaswa—ninapaswa kubatizwa kwa Roho Mtakatifu.” Sasa, haidhuru unaamini kiasi gani, huna budi *kutii* agizo hilo, unaona. Imani tu peke yake haitafanya kazi, kwa sababu “imani bila matendo imekufa.” Hiyo ni kweli.

29 Kama tu waaminio wakwamia mpakani, ninii tu, watu siku hizi, unakuta, katika Biblia inasema, "Kwa maana haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru, wakafanywa washirika wa Roho Mtakatifu, wakianguka, kujifanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kuihesabu Damu ya Agano, ambao kwake alitakaswa, kuwa ni kitu ovyo, na kuidharau kazi ya neema."

30 Sasa, katika Waebrania 10 pia inasema, "Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai."

31 Nao watu hao, mmewaona wakija kanisani, watakuja nao watasema, "Loo, naam, ni—ninaamini. Naam, bwana. Mimi . . . "

32 Lakini wataninii, wanaamini hilo, bali kamwe hawataweka mikono yao juu yake kuzungusha gurudumu moja kulisaidia liendelee. Mnaona? Sasa, hivyo ni kama tu ilivyokuwa katika Biblia, kama vile Kalebu na Yoshua walivyorudi na ushuhuda kwamba walikuwa kwenye hiyo nchi, lakini hao waumini wengine, walisema, "Loo, ni kubwa mno, hatuwezi kufanya hivyo." Lakini walishikilia vivyo hivyo, kamwe hawakupata kuingia katika nchi ya ahadi, ni wale tu waliorudi wakiwa na imani kwamba tungeweza.

Sasa, vipi kama kundi hilo lingaliangalia? Sasa, wao walisema, "Mbona, Wa—Waamori, na kadhalika, mbona, tunaonekana kama panzi kwao!"

33 Vema, lakini mnaona, Kalebu na Yoshua waliwatuliza hao watu, kwa sababu hawakuwa wakiwaangalia Waamori, jinsi walivyokuwa wakubwa, jinsi miji hiyo ilivyokuwa mikubwa, bali walikuwa wakiangalia ahadi, Mungu alisema, "Nimewapa hiyo nchi, ni yenu." Sasa, Mungu anawapa uponyaji wenu, kila mmoja wenu, ni wenu.

34 Vema sasa, Mungu hakwenda tu kule, akachukua ufagio, na kufagilia mbali Kanaani, na Waamori wote, na Wahiti, na—na hao wote, na kuwafagilia mbali, kasema, "Ingieni ndani Israeli, hii ni yenu, hata tumewapandia mimea."

35 La, bwana, iliwabidi kupigania kila inchi ya njia, hiyo ni kweli, bali walikuwa na ahadi ya ushindi, Mungu alimwambia Yoshua, "Popote zitakapokanyaga nyayo za miguu yenu, nimewapa ninyi." Kwa hiyo alama za miguu zilimaanisha umilikaji. Kumbuka hilo, dada kwenye kiti cha magurudumu. Nyayo za miguu zinamaanisha umilikaji, kila wakati nyayo za miguu yako zinapogusa, ndiyo hiyo, chukua ardhi kiasi hicho.

36 Wasema, "Nisingeweza kutikisa kidole changu jana, bali ninaweza kukitikisa leo." Umemiliki kiasi hicho, endelea tu kusonga mbele, naam, endelea tu kusonga mbele. Kesho unaweza kuutikisa mkono wako, kesho yake dhiraa zako, ndipo muda si muda wajua, wewe huyo unaenda. Endelea tu mbele, unaona. Nyayo za miguu ni umilikaji.

37 Unapofikia kwenye utii mkamilifu, basi unaweza kuwa na umilikaji. Lakini mpaka utakapotii kabisa! Inakubidi kusalimisha kabisa mawazo yako mwenyewe, mapenzi yako mwenyewe, nia yako mwenyewe, na uache nia ya Kristo itende kazi ndani yako.

38 Sasa, unafikiri Kristo angeninii, nia ya Kristo, ndani yako, ingesema, "Siku za miujiza zimepita"? Unafikiri nia ya Kristo ndani yako ingesema, "Biblia ni sahihi sehemu fulani, wala si katika zingine"? Nia ya Kristo ingeidhinisha kila Neno ambalo Kristo aliwahi kusema, ni kweli. Kwa hiyo kama. . .Hutumii akili yako mwenyewe, tumia tu nia Yake.

39 Hivyo ndivyo maono wakati wa usiku, kama nikitumia akili yangu mwenyewe, vipi, ningefanya nini? Nisingeweza kufanya lolote. Lakini kujisalimisha tu Kwake, na ndipo Yeye anatumia akili yangu, macho yangu, kinywa changu. Yeye ni yote kwangu, najisalimisha tu, hivyo ndivyo unavyofanya.

40 Hivyo ndivyo wahudumu hawa wanavyofanya wanapohubiri Injili. Wanapanda pale juu na kuchukua somo, mbona, wanaanza tu kuhubiri na kujitolea kwa Mungu, wao ni wahudumu, muda si muda mwajua Roho Mtakatifu labda awaongoze kwenye fungu lingine, awapeleke mahali pengine.

41 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham," kasema, "kamwe hukai kwenye somo lako, unapaswa kukaa kwenye barabara kuu."

42 Nikasema, "Kila mtu ninayemhubiria haishi kwenye barabara kuu. Inanibidi kushuka kwenye ujia wakati mwingine kumwokota mmoja *hapa* chini, mahali fulani. Kwa hiyo sina budi kuondoka kwenda mahali pengine, mahali tu aniongozapo."

43 Hivyo karibu ndivyo inavyoendelea, sivyo, ndugu? Inakubidi utoke kwenye barabara kuu mahali fulani, na kushuka upande *huu*, na kumwokota mmoja *hapa*, na *hapa*. Hujui unalisema, bali unafuata tu jinsi Yeye anavyolisema, anazungumza na mtu fulani *huko* juu, *hapa* chini, *kule*, mahali fulani, ni kwa ajili yao, kama tu ukifuata mwongozo Wake.

44 Sasa kwa hiyo, na hatimaye tunaona wakati Ibrahimu alipofikia kwenye utii mkamilifu, na akaja mahali alipokuwa, kila kitu kimeondolewa njiani, baba yake akafa, Lutu akajitenga na Ibrahimu, ndipo Mungu akamwambia Ibrahimu, "Ondoka utembee nchini, yote ni yako." Loo, na—napenda hilo! Kila ninapowazia hilo, ninapata hisia ya kidini mara tu ninapofanya hivyo. Mnaona? "Ondoka utembee nchini, kwa sababu unaimiliki yote."

45 Hivyo ndivyo tunavyofanya na Biblia hii. Mara tunapokuwa Wakristo na kujazwa na Roho Mtakatifu sisi ni Uzao wa Ibrahimu na warithi wa kila ahadi. Kwa hiyo tembeeni tu kote nchini, kila sehemu yake ni yenu, mwone mlicho nacho. Angalia kama Roho Mtakatifu ni yeye yule leo kama alivyokuwa jana,

angalia kama kila kitu ambacho Mungu aliahidi si vile vile, unaona, ni chako.

46 Wakati Kristo alipokufa, mnajua alilofanya? Alikupa kitabu cha hundi ulipofanyika mtoto Wake. Na chini ya kila hundi ina Jina la Yesu. Sasa, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kutia sahihi hundi hii pamoja Naye. Hakika, huogopi ati Yeye hatatimiza—Yeye hatatimiza Neno Lake, ati Benki ya Mbinguni haitaiheshimu, "Mwombe Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Loo, jamani, ni ahadi ya jinsi gani!

47 Je, wewe...? Ungeweza kuandika jina lako kwenye hundi pamoja Naye, usiku wa leo? "Kwa kupigwa Kwake, niliponywa. Mimi, William Branham, niliponywa, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, kwa kupigwa Kwake." Yeye ameandika Jina Lake katika Damu Yake Mwenyewe hapo chini yake, Baba atalitambua hilo, hebu lijaribu tu mara moja. Usilijaribu, lifanye tu. Mtu yeyote anaweza kujaribu, inahitaji mtu anayejua wanalofanya kulifanya. Hiyo ni kweli. Si *kujaribu*, hatuendi kujaribu. Kama una imani, hujaribu, nenda ukalifanye, kwa sababu unajua unaweza.

48 Kwa hiyo Ibrahimu alipotii naye akapata baraka, Mungu alisema, "Sasa umefanya tu yale niliyokwambia, tembea kote nchini, kila sehemu yake ni mali yako."

49 Na ndipo tuliona, baadaye, jana usiku katika somo letu la Ibrahimu, tunapomleta mahali alipopaita Yehova-yire, tunaona, humu ndani, ya kwamba Ibrahimu alifikia mahali pengine ambapo Mungu alitaka kulithibitisha agano hili.

50 Sasa, kama mkiangalia, ninataka kusimama tu kwa ajili ya msingi wa mahali ninapoelekea, Mungu sikuzote hutoa ishara na maajabu ya thibitisho la ahadi Zake.

51 Sasa, ni wangapi hapa ndani ambao wamempokea Roho Mtakatifu? Inua mkono wako, walio Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Hilo ni thibitisho ya kwamba Yeye angali ni Mungu. Hiyo ni kweli? Hilo ndilo thibitisho Yeye angali ni Mponyaji. Mtu angewezaje kamwe kuhubiri uponyaji wa Kiungu bila kuhubiri, uh, kuhubiri neema ya Kiungu bila kuhubiri uponyaji wa Kiungu? Sijui mimi.

52 Ugonjwa ni nini? Ugonjwa ni sifa ya dhambi. Kabla hatujawa na ugonjwa wowote, hatukuwa na dhambi. Dhambi huja kama matokeo ya ugonjwa, labda si dhambi yako, bali dhambi ya wazazi wako. Kama tu vile ulivyopewa ulipozaliwa, na kadhalika.

53 Sasa, si lazima uninii tu, kama joka kubwa, ama—ama mnyama, kama simba alikuwa amechomelea makucha yake ubavuni mwangu, ilikuwa ni uvimbe ama kansa, ikijaribu kuniua, hakuna haja ya kujaribu tu kukata mguu wake kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu, kama ukimgonga tu kichwani inaua kitu hicho chote.

54 Basi wakati Yesu alipokufa kwa ajili ya dhambi, Yeye alikufa kwa ajili ya kila sifa ambayo dhambi iliwahi kutoa. Mnaona? Kwa hiyo wakati dhambi ilipokwisha, *yote* ilikwisha, mpango kamili wa ukombozi. Kwa hiyo sisi ni . . . Unampiga tu kichwani kwa swali la dhambi, ukiua dhambi, unaua kila sifa. Unaona?

Unasema, "Dhambi ni nini?"

55 Kutokuamini. Kwa hiyo unapoua kutokuamini kwote, mbona, unajua ya kwamba Neno la Mungu ni kweli, ya kwamba ni yeye yule jana, na hata milele, kwa hiyo ahadi zote ni zako. Tembea kote nchini, yote ni yako, ni mali yako. Ifurahie tu, ni yako, Mungu alikupa wewe, neema ya Mungu ilikupa wewe, yote ni yako. Hapo swali la dhambi linapokwisha, umempokea Roho Mtakatifu, kila kitu unachohitaji katika safari ya maisha kiko pale pale katika Biblia kwa ajili yako, kila kitu unachohitaji.

56 Leo, kuna mwanamke aliyeketi mkutanoni usiku wa leo, mke wa mhudumu aliyeshuka kutoka Tacoma, nami nilikuwa na mahojiano mafupi na mwanamke huyo leo, huku ameketi pale. Huyo mwanamke alikuwa na jambo fulani, madaktari walikuwa tayari wamesema, kitu fulani *hivi-na-hivi* kwake, na kitu fulani mle ndani, naye alikuwa—naye alikuwa akijiandaa kufa.

57 Naye Roho Mtakatifu, akiketi moja kwa moja chumbani, akaja moja kwa moja na kufunua jambo hilo, na mara tu Hiyo ilipomgusa huyo mwanamke, aliangua kilio kikuu, naye, kwa furaha, akaponywa. Mungu aliugusa mwili wake na kumponya.

Uko hapa, Dada Rasmussen? Uko wapi? Uko hapa jengoni, mahali fulani? Ameketi nyuma *kule*. Naam, bwana.

58 Sasa, Roho Mtakatifu aliingia chumbani, na kufunua jambo hilo, akalifungua. Hakukuwa na njia ya . . . Sikumwombea, haikunibidi kumwombea. Unapoijua kweli, hiyo kweli inakuweka huru. Loo, napenda hilo. Nanyi je? Kweli inakuweka huru.

59 Unapojua ya kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako, nawe umemkubali kama Mwokozi wako, unaye Roho Mtakatifu, na kwa kupigwa Kwake uliponywa, kama unajua kweli hiyo, hiyo kweli pekee, inakuweka huru. Amina. Hakuna haja ya maombi, haikuninii . . . si kuomba, ni kuamini tu, kuamini ile kweli.

60 Wakati mwingine inatubidi kuomba kuiingiza kweli hiyo mioyoni mwetu, bali Mungu alitupa kila chombo, karibu hivyo, kilichoko cha Ufalme wa Mungu cha kufanyia kazi, kuleta imani kwa watu, karama, ishara, maajabu, kila kitu cha kufanya hivyo. Lakini anapofanya hilo, basi ni kazi iliyomalizika; Mungu alifanya hivyo. Wakati Yeye—wakati anapokufanyia hilo, nawe unaliamini, unalikubali, basi uponyaji wako umekamilika, ni hayo tu. Huna budi kuamini Neno la Mungu.

61 Sasa napitia kwenye kinjia kingine, kwa dakika moja tu. Lakini hivi majuzi, nilikuwa na mkutano katika mji fulani, na kulikuwa na mama mmoja aliyekuja jukwaani akiwa na ugonjwa wa tumbo. Roho Mtakatifu akamwambia, kasema . . . Loo, inatukia tu mara mia kadhaa katika kipindi cha miezi michache. Akamwambia, alikuwa na ugonjwa mbaya sana wa tumbo, akamwambia yeye alikuwa ni nani, alikotoka. Hayo yote yalikuwa ni kweli. Kisha kasema, "Uliugua ugonjwa huu wa tumbo kwa muda mrefu."

62 Akamwambia ilikuwa ni ugonjwa wa aina gani ya vidonda, na yale madaktari walikuwa wamesema, aina ya madaktari waliomshughulikia, hayo yote yalikuwa ni kweli, ndipo akaanza kuondoka jukwaani, sasa, inakubidi kuangalia hilo, unaona, na ndipo alipoanza, nikaona ono lingine. Mnakumbuka, wakati huo ni BWANA ASEMA HIVI. Nikamwambia, "Nenda ukale, kwa kuwa BWANA ASEMA HIVI, umepona."

63 Akashuka mstarini, akapitia humo. Akaenda nyumbani usiku huo, na ilikuwa ni mmoja wa majirani zake aliyeondoka na alikuwa na uvimbe mkubwa kando ya shingo yake, kama uvimbe wa mafuta moja kwa moja chini ya kidevu *hapa*, ama mfupa wa taya, na mtulinga *hapa*, uvimbe mkubwa karibu umetokeza inchi moja au zaidi. Basi Roho Mtakatifu akamwambia jambo lile lile, "BWANA ASEMA HIVI, umepona."

Vema, usiku huo wakienda nyumbani, walikuwa kwenye gari lile lile, kwa hiyo wakazungumzia jambo hilo, vema, wakasema, "Labda, itakuwa, tu—tutakuwa sawa."

64 Vema, huyo mama akaenda nyumbani, nami nikamwambia, Roho Mtakatifu akamwambia, hasa, aende zake kwamba aliponywa, kwa hiyo akaenda nyumbani, akawazia labda angeweza kula. Jamani, ikamfanya mgonjwa sana! Na kwa hiyo basi kesho yake, akaendelea huku majuma mawili ama matatu yakapita naye hakupata nafuu.

65 Na kwa hiyo mume wake akamwambia, kasema, "Sasa, mpenzi, sijali wewe kutoa ushuhuda, lakini," kasema, "kumbuka tu," kasema, "hujapata nafuu." Kisha kasema, "Huna budi . . . Unailetea huduma lawama, hapo u—unaposema hivyo." Kasema, "U—unasema ya kwamba umepona wakati hujapona."

66 Akasema, "Angalia, Mpenzi," akasema, "mtu huyo kamwe hakunijua. Alinijuaje wakati tunaishi maili mia moja na hamsini kutoka mahali ambapo hajawahi kuwa?" Kisha kasema, "Aliniambia kweli kabisa, neno kwa neno, nawe unajua hilo." Kisha kasema, "Halafu—halafu, nilipoanza kuondoka jukwaani, aliniambia, 'BWANA ASEMA HIVI, umepona.'" Kasema, "Kama nikitumia miaka mingine hamsini nikilishuhudia bila matokeo yoyote, bado nitasema nimepona." Kwa hiyo hilo—hilo ndilo, hilo ndilo wazo. Alikuwa nao.

67 Na kwa hiyo, siku chache baadaye, alikuwa, asubuhi moja alikuwa amesimama akiosha vyombo, watoto walikuwa wameenda shuleni, na—na mumewe alikuwa ameenda kazini, naye alikuwa akiosha vyombo kwenye—kwenye dirisha, naye akasema kama tu hisia baridi ilipitia juu yake. Na *kwa namna fulani*, aliendelea, kamwe hakuliona, labda tu kama mtetemo mdogo ama chochote kile, mwajua, naye akasema aliendelea tu na kuosha vyombo.

68 Kasema dakika chache alishikwa na njaa sana, njaa sana ilikuwa vigumu kwake kuistahimili. Na shayiri sikuzote ilimchefua, mwajua vile shayiri inavyofanya kwa kidonda. Kwa hiyo, akala vijiko kadhaa vya shayiri kutoka kwenye sahani za mmoja wa watoto, akaimeza, ndipo akawazia angeendelea. Kasema, "Ninajua nitakitapika, labda, katika dakika moja," kwa maana sikuzote alitapika, maana kilirudi moja kwa moja juu. Na kwa hiyo, akashuka akala hiki, naye akaanza, kamwe hakikumsumbua, hakikumchoma. Vema, akarudi na kumaliza hiyo sahani. Kwa hiyo, muda si muda mwajua, alikuwa amesimama pale kwa dakika chache, hakuna kilichotukia.

69 Mnaona, kuamini kwake kulikuwa kumekwisha basi, haikumbidi kuamini basi, ilikuwa tayari imetendeka. Mnaona? Wewe amini tu *mpaka*, mpaka litakapotimia, ndipo unajua. Kwa hiyo basi, kazi yote imekwisha. Hivyo ndivyo ono lilivyo, linaposema jambo fulani litatukia basi unaamini tu mpaka hilo litukie, ndipo imekwisha. Unaona? Unaamini litatukia, wakati tayari limetendeka, limekwisha.

70 Kwa hiyo basi, baada ya kitambo kidogo akaona, alingojea yapata nusu saa, wala hakuna kitu kilichotukia, alikuwa na njaa tena, akakaanga mayai kadhaa, akajitwalia tosti, akajitengenezea kikombe cha kahawa, naye alikuwa na yubile ya maakuli, alikuwa tu na wakati mzuri. Naye akangojea yapata, kufikia yapata saa nne naye, loo, mambo yalikuwa barabara kabisa, anaona njaa tena. Kwa hiyo, akafurahi sana, akasema, "Nitashuka mbio kule chini," na kumwambia jirani yake.

71 Naye, alipofika karibu sana na hiyo nyumba, alimsikia mtu akipiga mayowe kule kwa sauti yao yote. Ndipo akakimbia mlangoni, na kufungua mlango upesi, ambapo mwanamke huyu ameshika shuka mkononi mwake, akilitikisa hilo shuka, akienda huku na huku sakafuni. Kasema, "Kuna nini?"

72 Yule mwanamke aliyekuwa na uvimbe shingoni mwake, akasema, "Unajua nini?" Kasema, "Asubuhi ya leo niliamka na ule uvimbe umekwisha! Nimetafuta kote kitandani, nimekung'uta mashuka na kila mahali, siwezi kuupata, popote." Mnaona?

73 Nao wakaja yapata maili mia tano kushuhudia hilo. Ilikuwa ni kitu gani? Malaika wa Bwana alipitia huo ujirani asubuhi hiyo. Mnaona? Wakati mwingine Mungu hawezi kujibu kwa

wakati huo. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Danieli aliomba, na ilikuwa siku ishirini na moja hapo kabla? Mnakumbuka hilo? Hakika. Lakini Mungu anaposema jambo lolote, Mungu hudumu na Neno Lake, wewe dumu Nalo, pia. Lakini ukiliacha Neno, unamwacha Mungu, unaacha—unaacha baraka zako, na kila kitu pale, dumu na ulitii Neno la Mungu. Yale Mungu asemayo, Mungu hufanya.

74 Na hivyo ndivyo ilivyombidi Ibrahimu kufanya, kwa hiyo basi Mungu akalithibitisha pamoja naye. Nasi tulipitia jana usiku ule utaratibu mzuri wa thibitisho, na jinsi ambavyo huko Mashariki, na jinsi Mungu alivyompasua Kristo vipande viwili, na kuupandisha Mwili Wake hata kwenye mkono Wake wa kuume, mkono wa kulia, hasa, na kumtuma Roho Mtakatifu juu ya Kanisa ku—kuwatia mafuta wana na binti wengine wa Mungu. Na Roho yuyo huyo aliyekuwa juu ya Kristo yuko Kanisani sasa. Mnaamini hilo?

75 Angalieni, nina jambo la kusema, lakini na—na—nahofia litaeleweka vibaya. Hebu tuchukue pembetatu, tuseme namna *hii*, sasa tutaanzia chini, hayo yalikuwa matengenezo ya kwanza, Martin Luther. Loo, lilikuwa—lilikuwa ni jambo baya sana hata kusema ulikuwa Mkristo wakati huo, kwa sababu uliteswa, na kudhihakiwa, na kadhalika. Kumbukeni, mwenye haki sikuzote huteswa, daima ameteswa, na daima atateswa.

76 Sasa kwa kuwa, tulikuwa na nafasi kubwa sana, kuhesabiwa haki kwa imani tu, huko kuliendelea kwa muda, mpaka tukawa na Calvin, na Knox, na kadhalika. Ndipo baada ya kitambo kidogo akaingia John Wesley akiwa na ujumbe mpya wa utakaso, Kanisa likawa katika uchache. Ndipo Wawesley wakaunda madhehebu, nao wakaunda madhehebu ya kila namna, kisha wakaja Wabaptisti, na Wakampbeli, na kadhalika, baada ya hapo, mpaka hatimaye, muda si muda mwajua, ikaanza kufumuka.

77 Na sasa angalieni, linakaribia zaidi wakati wote, kama tu piramidi, mnaona, likikaribia wakati wote, Kanisa likiingia katika uchache. Ndipo baada ya Wawesley kufia kwenye utakaso, moja kwa moja wakaja Wapentekoste pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kule kurudishwa kwa karama. Sasa, sasa linafikia katika uchache, mnaona, tena, likishuka. Sasa, litaninii . . .

78 Sasa, Roho wa Mungu alikuwa ndani ya Walutheri, Roho wa Mungu alikuwa ndani ya Wesley, na Roho wa Mungu alikuwa ndani ya Wapentekoste. Lakini ni kitu gani? Kanisa la Kipentekoste ni kanisa la Kilutheri lililoendelea mbele, hivyo tu, ni kanisa la Kilutheri lililoendelea mbele. Sasa, linapofikia *hapa*, Kanisa litapaswa kuwa katika utaratibu *kama* huo.

79 Kama umewahi kuwa Misri, utajua ya kwamba ile piramidi kuu huko Misri ambayo wote wanaizungumzia sana, ambayo

wengi wanadai kuwa ni kitu cha kinabii kilichojengwa kabla ya yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika, hilo nisingeweza kusema, sijui lolote kulihusu, lakini kama ilikuwa hivyo, basi jiwe la kichwa halikuwekwa kwenye piramidi hiyo. Walipata, kasema walilipata katika nchi mbalimbali, na kadhalika, bali kamwe lisingetoshea kwenye ule mchoro unaolingana na ma—mawe yaliyokuwa kule juu. Ingebidi itengeneze, hicho kifuniko kule ingebidi kiwe ni jiwe kamilifu. Kama ina mfano wowote wa unabii, basi lile jiwe la kichwani lilikataliwa kama tu vile lile Jiwe kuu la Pembeni la Biblia lilivyokataliwa.

80 Lakini sasa, kama tunakaribia zaidi na zaidi, naye Roho wa Mungu amekuja kutoka kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, Kanisa itabidi liwe karibu sana, na Roho wa Mungu akifanya kazi kikamilifu sana katika Kanisa hilo, hata wakati Jiwe la Kichwa litakapokuja, litalifunika pamoja, nao ufufuo utakuja, na Kanisa litaondoka.

81 Sasa, huo—huo ni uvumi tu. Mnaona? Lakini ni—ninajaribu kuwaonyesha jambo fulani ambapo Kanisa halina budi kufikia mahali lipate kuwa na Roho wa Kristo ndani Yake, Roho wa Kristo akitenda kazi katika miili yetu, kama tu alivyotenda kazi katika Mwili wa Bwana wetu. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya; nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu."

82 Sasa, hiyo ilikuwa ni ahadi ya Mungu ambapo alimpa thibitisho baba yetu, Ibrahimu, nasi tukiwa wafu katika Kristo tunachukua Uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi kulingana na ahadi. Basi kama sisi ni Uzao wa Ibrahimu, Roho Mtakatifu anaishi ndani yetu, akifanya kazi za Kristo. Mnaona ninalomaanisha?

83 Sasa angalieni, tunapoanza kukaribia, hebu tumpeleke Ibrahimu mbele kidogo, tutalifikia. Kujua tu. . .Tulikuwa katika mlango wa 15 jana usiku, ama, wa 16, sasa usiku wa leo hebu na turuke kwenye mlango wa 17, kifungu cha kwanza wakati Mungu alipomtokea Ibrahimu basi baada ya kupata umri wa miaka tisini na tisa, tisini na tisa, katika mlango wa 17 wa Mwanzo.

84 Sasa, alipomtokea pale, alimtokea katika Jina la Mwenyezi Mungu. Neno la Kiebrania hapo linatokana na neno la El Shaddai. *El* "mwenye nguvu," Shaddai, *shad* linamaanisha "titi la mwanamke," bali *Shaddai*, *Shaddai*, linamaanisha wingi, "mwenye matiti." Yeye ni Mungu mwenye matiti.

85 Hilo si lilikuwa ni la kushangaza sana kwa mzee mwenye umri wa miaka mia moja, ambaye ni kama aliyekufa, mkondo wa maisha yake ulikuwa umekwisha, tumbo la uzazi la Sara limekufa kwa miaka mingi, m—mke ana umri wa miaka tisini, yeye ana umri wa miaka mia moja, ndipo Mungu akamtokea kama El Shaddai? "Mimi ni Mungu mwenye matiti." Loo,

jamani! Angalieni, sio tu Mungu-matiti, bali Mungu mwenye matiti.

86 Loo, ninyi msioamini katika uponyaji wa Kiungu, natumaini hili linasaga ndani sana. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa." Unataka wokovu kwa ajili ya nafsi? Titi *hili*. Kama unataka wokovu kwa ajili ya mwili, titi *hili*. Yeye ndiye El Shaddai, Mwenyezi, Mwenye nguvu.

87 Si kwamba tu mwanamke. . . Titi lake ni la kumnyonyesha mtoto wake; titi la Mungu ni la kuwanyonyesha watoto Wake. Hebu mchukue mtoto mchanga, mgonjwa wakati ni mgonjwa sana na anahangaika, mama anaweza kumchukua huyo mtoto mchanga, akamvuta mpaka kifuani mwake, naye ananyonya nguvu zake kutoka kwa mama yake. Amina. Loo, unaliona, ndugu? Unaona, kama sisi ni wagonjwa, tumjie tu El Shaddai. Amina. Shikilia, nyonya nguvu na afya yako kutoka Kwake. Yeye ni El Shaddai. Amini hilo, dada, msichana huyo mrembo, aliye kwenye kitanda cha wagonjwa.

88 Vema. Iweni na imani kwake, liaminini, mshikilieni tu El Shaddai, Mungu mwenye matiti. Sio tu kwamba mtoto mchanga hupata nguvu za—zake kutoka kwa mama yake, bali pia huacha kuhangaika, ameridhika. Yeye ni Mridhishaji. Mtoto mchanga anapoanza kunyonya ngu—nguvu za mama katika mwili wake mwenyewe, anaridhika wakati anaponyonya. Amina. Haya basi!

89 Sasa, kama tumemshika Mungu kwa imani, na kuamini ya kwamba Yeye ndiye Mpaji nguvu: "Kwa mapigo Yake niliponywa, ninaikubali kama mali yangu. Kila ahadi ni yangu. Agano limethibitishwa kwa kunipa Roho Mtakatifu na kunijaza na wema Wake na rehema, kuniokoa na dhambi, kugeuza kichwa changu kutoka kwa mambo ya ulimwengu, na kuweka upendo wangu Kalvari. Sasa, ninajua hiyo ni kweli. Nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Jambo fulani lilinipata ambalo lilibadilisha utu wangu wote." Miaka thelathini na mmoja ambayo imekuwa mitamu na muhimu kwangu, ni bora zaidi usiku wa leo, kuliko ilivyowahi kuwa. Ninajua ya kwamba jambo fulani lilinipata.

90 Vema. Yeye yule anipaye furaha, na nguvu, na wokovu amesema, "Kama wewe ni mgonjwa njoo moja kwa moja kwenye titi hili lingine unyonye nguvu zako kutoka Kwangu." Loo, jamani! Umeridhika, inaridhisha. Ninaposikia Neno la Mungu likisema kwa kupigwa Kwake niliponywa, hilo linaniridhisha. Amina. Hiyo ni kweli. Usihangaike tena, usikimbie tu kutoka *hapa* hadi *pale*, usifanye *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*, la—lala tu hapo na kunyonya nguvu na afya yako tena kutoka kwa El Shaddai, Mwenye nguvu.

91 Mara nyingi watu wamekuja, nimekuwa kwenye hospitali za wendawazimu kuangalia, na linasikitisha sana jinsi walivyo, na mara nyingi, wakati nanii, Shetani anapowashika watu hao,

ambao, mara nne au mara tano ya nguvu zao, mwendawazimu ana mara nyingi ya nguvu zake. Hebu mwangalieni yule—yule—yule mwendawazimu wa Gadara, mbona, wakimfunga minyororo, angeivunja, hakuna mtu angaliweza kumdhibiti, pepo walikuwa na jeshi zima ndani yake. Sasa, kama jeshi la pepo ndani ya mtu linaweza kumpa mara nne au tano ya nguvu zake, Roho Mtakatifu atafanya nini atakapomshika mtu?

92 Haidhuru kama yeye ni mgonjwa, kama anateseka, unasema, "Vema, kamwe siwezi kusogea," hebu Roho Mtakatifu ashike wakati mmoja, na uone kitakachotukia. Naam, bwana. Loo, inaninii tu, inaongeza nguvu zako maradufu na mara tatu, maana hutembei katika nguvu zako, unatembea katika nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo. Mungu alimfufua katika wafu, na kuyafungua maumivu ya mauti, na kumkabidhi kwetu kama upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, nasi tu—tunajua ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, nasi tutapata tuombacho.

93 Labda, ni wakati mmoja tu wa uuguzi, hupati nguvu za kutosha, kaa tu hapo, nyonya kutoka Kwake mpaka utakapotembea, mpaka kansa imekwisha. Kataa kuona kansa, kataa kuona chochote ambacho ni kinyume na Neno Lake, sivyo ilivyo. Kila kitu, kama Yona, "Huo ni ubatili wa uongo. Hata sitayaangalia, sitayatambua. La, bwana, ninaona yale Mungu aliyosema." Msiwaone Waamori, msiyaone makaburi, msiyaone mambo haya, angalieni ahadi ya Mungu. Mungu aliahidi jambo hilo, ni juu ya Mungu kulishughulikia. Naam, bwana.

94 Sasa, ninajua ya kwamba mauti hayana budi kumgusa kila mtu, mauti yanatujia sisi sote, lakini wakati mwingine, kwa sababu tu ya kutokuamini tunakata tamaa na kwenda kwenye kaburi la mapema. Mungu hataki tufanye hivyo, Anatutaka tumwamini, na kumwamini Yeye, na—na kusema ndivyo ilivyo, na kudumu nalo, kwa sababu Mungu . . .

95 Lazaro alikufa, hiyo ni kweli, alifufuka tena, na akaishi maisha ya kawaida kwa miaka mingi, mingi sana, kwa sababu ya ufufuo aliopewa na Yesu. Halafu basi, bila shaka, alikufa tena, kwa sababu atatokea katika ule ufufuo. Yesu alisema angefufuka katika ule ufufuo, bali hana budi kwenda kwenye raha yake, kama wanadamu wote. Lakini mpaka wakati huo utakapokuja, hebu na tusidanganyike tukaacha maisha ya kumtumikia Mungu, maana ni kazi ya Shetani kukudanganya uyaache. Naam, bwana. Lakini Mungu ni El Shaddai, amina, Mwenye nguvu, Mungu mwenye matiti, Mwuguzi, M—Mwenye kuwapa nguvu watoto Wake wagonjwa, watoto Wake wanapokuwa wagonjwa.

Unasema, "Vema, nina umri wa miaka tisini."

96 Vivyo hivyo na Ibrahimu, alikuwa na umri wa miaka tisini na tisa, bali alikuwa angali ni mtoto mchanga, Mungu akasema,

"Liegemee titi Langu unyonye, Ibrahimu." Amina. Miaka tisini na tisa ilikuwa nini kwa Mungu?

97 Unajua sabini yako inamaanisha nini kwa Mungu? Kulingana na wakati, Yeye hana wakati, Yeye yuko katika Umilele, bali ile miaka elfu, nafikiri, ni kama dakika tatu ama nne za wakati wa Mungu, umeninii. . .umetwaliwa pamoja nawe, maisha yako yote, kwa karibu miaka mia moja.

98 Kwa hiyo, Ibrahimu hakuwa kitu ila mtoto mchanga tu, ndipo Mungu akasema, "Panda hapa juu, Ibrahimu, wewe ni mzee, una umri wa miaka mia moja," masharubu yalikuwa yamening'inia chini namna *hii*, nywele zenye mvi, nazo. . . "Wewe ni m—mzee sana kwa ulimwengu, lakini kwangu Mimi wewe ni mtoto tu. Wewe ni mtoto tu, Ibrahimu, panda hapa pajani Mwangu, keti hapa chini u—ukanyonye kurudisha nguvu zako." Loo jamani!

99 Na kila kitu alichompa Ibrahimu, kwa ahadi, alimpa Ibrahimu na (*Na* ni kiunganishi.), na Uzao wake baada yake. Amina. Hivi hamna furaha kwamba ninyi ni Uzao wa Ibrahimu? Loo, nina furaha sana! Loo, ninajisikia kuimba wimbo ule:

> Kila ahadi katika Kitabu ni yangu,
> Kila sura, kila kifungu, kila mstari.
> Ninatumainia upendo Wake wa Kiungu,
> Kwa maana kila ahadi katika kile Kitabu ni
> yangu.

100 Ni yako. "Yeyote atakaye, na aje anywe kutoka kwenye chemchemi ya Maji ya Uzima bure." Ni kwa yeyote atakaye anaweza kuja.

101 Kwa hiyo, Mungu alimfanyia Ibrahimu jambo hili, naye Ibrahimu akiwa na umri wa miaka mia moja, na Sara umri wa miaka tisini. Maskini bikizee sasa, inawezekana alikuwa na shali ndogo begani mwake, na maskini kofia ya mavumbi, ameegemea fimbo ndogo, akitembea namna *hii*.

102 Vema, yapata siku chache baadaye, alikuwa ameketi kwenye jua kali asubuhi moja, na loo, hapana shaka ulikuwa ni wakati wa kutisha sana. Tuko—tuko kwenye yapata mlango wa 18 sasa, na kwa hiyo, wa 19. Alikuwa ameketi nje kwenye jua kali, mchungaji akaja, na kusema, "Loo, jamani," walikuwa wakipiga makelele, "maji yote yamekwisha," na kila kitu kilionekana kana kwamba kilikuwa kikienda mrama. Angalieni wakati hilo linapotukia, kwa Mkristo, hilo linapotukia kuna baraka iliyo hapo mbele tu, naye Shetani anajaribu awezavyo kuiweka mbali na wewe. Nimeona jambo hilo maishani mwangu.

103 Ninapoenda kuomba, nitaenda huko mwituni, yungiyungi-mwitu (Hamna hiyo hapa, sivyo? Lakini tunayo nyingi huko mashariki.), nayo inakukwaruza; halafu unahamia *hapa*, nalo jua linakuangazia kupitia kwenye miti; ukienda *huku*, ni

ubavuni mwa kilima, unaomba namna *hii*; na *huku* kuna mawe mengi kupita kiasi, na mbu wanakuuma, na loo, kila kitu.

104 Sasa, unapofikia mahali kama hapo, inua tu mikono yako juu, na kusema, "Haleluya! Mungu, Wewe unaniita, nami ninakujibu." Jambo fulani litatukia, hiyo ni kweli, maana kuna baraka iliyowekwa pale, na Shetani anajaribu kupiga vita, yeye ni maskini mwenye mguu uliopasuka, kwa vyovyote vile, mwajua, naye—naye anajaribu awezavyo kukuzuia usiingie kwenye baraka hiyo. Kaa tu hapo mpaka utakapoomba ufanikiwe, sijali, acha mbu waume, lolote linalotukia, dumu tu nalo, maana Shetani atakunyang'anya hilo kama akiweza.

105 Kwa hiyo huyu hapa Ibrahimu, ninamwona baada ya Mungu kumtokea kama El Shaddai, anarudi, na kusema, "Sara, unajua nini? Mimi ni mtoto mdogo tu."

Akasema, "Kwa kweli, Ibrahimu, ndivyo ulivyo?"

"Naam, Naye aliniambia niegemee tu kifuani Mwake na kunyonya nguvu zangu tena." Hiyo ni kweli, alikuwa na umri wa miaka tisini na tisa.

106 Vema, alikuwa ameketi pale asubuhi moja, na muda si muda, waliangalia na kuona watu watatu wakija. Naye Ibrahimu, akiketi chini ya mwaloni huu, katika, katika mlango wa hema lake, aliangalia nje...Nanyi mwajua, kuna jambo fulani tu kuhusu Mkristo unaloweza kujua, kuna jambo *fulani* tu, unamjua Mkristo. Amewahi kumpokea Roho Mtakatifu, zungumza naye kwa sekunde moja, utajua jambo *fulani* limempata, amevuka akaingia katika nchi ya Kanaani. Kwa hiyo, mnamwona, ametiwa alama.

107 Nao hao hapo wameketi huko nje, ndipo hawa watu watatu wakaja, wamejaa mavumbi kwenye nguo zao, na kusema, "Sisi ni wageni, tumetoka Nchi nyingine." Naam, mbali sana: Utukufu.

108 Naye akasema...Ndipo Ibrahimu akaandaa vitu, na kumwambia Sara aoke mkate, kama tulivyofanya hivi majuzi usiku, na kuuleta, na kuuweka mbele yao, nao wakala. Wawili kati yao wakashuka kwenda Sodoma, kwa sababu Sodoma ilikuwa karibu tu ku—kuteketezwa.

109 Na sasa, Mmoja alizungumza na Ibrahimu. Nao hawa wakashuka na kumhubiria Lutu, Mchungaji Lutu huko chini Sodoma. Naye akajaribu alivyoweza kuwatoa hao watu, lakini wasingesikiliza, walikuwa wa kisasa tu kadiri watu hawa walivyo siku hizi katika taifa hili. Walikuwa na njia zao wenyewe, na dini zao wenyewe, na mipango yao isiyobadilika, nayo dhambi ilikuwa ikilundikana kila upande, nao—nao walikuwa na njia yao wenyewe, hata usingeweza kuzungumza nao.

110 Uliwahi kuwaona watu usioweza kuzungumza nao? Hakuna mtu, ungeweza. . .Huwezi kuwaambia chochote, maana hawataamini, watasikiliza tu kwa sekunde moja, wameondoka, hivyo tu. Wao. . .Jagi ndogo itajaa kabla ya ile kubwa, mwajua, na kwa hiyo basi hao wanaondoka, wala hawatasikiliza hata kidogo.

111 Sasa, basi kulikuwako na Yule aliyebaki nyuma na kuzungumza na Ibrahimu, ndipo Huyu akamwambia, "Ibrahimu, yuko wapi Sara, mkeo?"

112 Sasa, kwa kuwa tulikuwa na hili hivi majuzi usiku, nitalielezea kifupi tu kwa muda kidogo. Sasa, Yeye alijuaje alikuwa ameoa, alikuwa na mke, na jina lake lilikuwa Sara?

Ndipo Ibrahimu akasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

Akasema, "*Mimi* nitakuzuru, Ibrahimu. Nitatimiza ahadi Yangu."

113 Sasa, Mtu huyo alikuwa ni Nani? Nawatakeni mwone, Mtu huyo aliyekuwa ameketi pale akila alikuwa ni Nani? Vema, Yeye alikuwa akila vipande vya nyama ya ndama, ugali, siagi na mkate, akinywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, Mtu ameketi pale amejaa mavumbi kwenye nguo Zake, nayo Biblia ilisema ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Ibrahimu alimwita Elohimu. Angalieni hizo herufi kubwa, *Bwana*, Bwana, Elohimu, zifuatilieni mwone. Bila shaka, wachungaji hapa wanasema, "Amina," kwake kwamba ndivyo ilivyokuwa. Ilikuwa ni Elohimu.

114 Ndipo Yesu akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Elohimu, Yule mwenye nguvu, angeshuka katika mwili wa kibinadamu. Loo! Mnalipata? Elohimu, Yule mwenye nguvu, angeshuka katika mwili wa kibinadamu, na angejidhihirisha Mwenyewe kwa kujua siri ya moyo wa yule aliyekuwa akisema naye, jinsi hasa Mwanawe alivyofanya alipokuwa hapa duniani. Mnaona? Akiishi katika mwili wa kibinadamu. Mwili gani? Mwili wako, mwili wangu. Roho Mtakatifu, Mwenyewe, akishuka katika mwili wa mwanadamu na kukaa, akionyesha ishara, kasema, "Yu wapi Sara, mkeo?"

Kasema, "Yuko hemani nyuma Yako?"

Naye akasema, "Nitakuzuru."

115 Ndipo Sara akasema, "*Humph*! Mwanamke mkongwe kama mimi nipate raha na bwana wangu," Biblia ilisema wote wawili walikuwa na umri mkubwa, umri mkubwa sana, "kuwazia nina raha na bwana wangu tena," kwa sababu alikuwa, mbona, alikuwa amekoma hedhi kwa miaka arobaini na mitano, "kuwazia kwamba ningepata raha na bwana wangu tena, kwa kuwa mimi ni mkongwe, na bwana wangu ni mzee?" Akasema, "Hiyo isingewezekana kabisa."

Naye Malaika, Mungu katika mwili wa mwanadamu, akila nyama, akila mkate, akinywa maziwa, ameketi pale, akasema, “Kwa nini Sara akacheka?”

116 Loo, Yesu alisema jambo lilo hilo litatokea kabla tu ya Moto kuanza kushuka juu ya Sodoma na Gomora ya kisasa. Mnaona jinsi tulivyo karibu, enyi marafiki? Angalieni ile ishara kwa Kanisa.

117 Hebu nisimame hapa kidogo. Hivi majuzi, nilikuwa India, ambako Bwana alitupa mkutano mkubwa sana tuliowahi kuwa nao; tungeweza tu kukaa siku mbili. Hakuna mahali pa kuwaweka hao watu, waliokadiriwa kuwa laki tano mkutanoni, hao ni watu nusu milioni, hakuna mahali pa kuwaweka. Nje ya mipaka ya mji usingeweza kupata ulinzi, nao wangefanya ghasia, na kwa hiyo wasingeturuhusu kuufanyia huo mkutano nje. Tunapaswa kuwa, Oktoba hii, mwisho wa Oktoba hii kuwa New Delhi, kama ninaweza kuachiliwa niende, ambako tuna uwanja mduara ambao utaenea watu milioni moja, kwa hiyo kama nikifanya mkutano huko India.

118 Basi nilipofika huko, nilichukua gazeti, nalo likasema, “Lazima tetemeko la ardhi limekwisha.” Ninalo, makala yako nyumbani, samahani, Wafanyabiashara Wakristo waliyatumia wakayaandika katika, gazeti la—lao. Kwa hiyo mimi . . . Lilisema mle, “Tetemeko la ardhi halina budi kuwa limekwisha.” Kasema, “Siku tatu zilizopita, siku mbili kabla ya tetemeko la ardhi kuja . . . ”

119 Huko India, hawana nyua, waya uliofumwa kama tulio nao huku Washington na kote. Wao huokota mawe kondeni . . . Kuna watu mia nne na sabini, ama, watu milioni mia nne sabini India, na ilionekana kwangu kama milioni mia nne kati yao walikuwa ombaomba. Kwa hiyo, wao—wao wana rasilimali nyingi sana, bali hawana uwezo wa kiakili kuziendeleza. Kwa hiyo, wanaokota mawe na kujenga nyumba zao, wanaokota mawe na kujenga nyua zao.

120 Nao ndege wadogo wanaingia kwenye mawe haya na kujenga viota vyao, vema, na halafu jioni, ambapo hakuna kivuli, ng’ombe watasimama kuzunguka nyua hizi kubwa, ndefu wapate kivuli wakati jua ni kali sana. Lakini kwa muda wa siku mbili, hao ndege wadogo walikuwa wameacha maghuba haya yote madogo mle ndani kwa ajili ya viota vyao, na kwenda makondeni vichakani; ng’ombe wote, jioni, walikuwa wakisimama karibu na ua, na kondoo wote, na kadhalika, walienda moja kwa moja katikati ya uwanja na kuegemeana, wamesimama moja kwa moja kwenye jua kali.

121 Watu hawakujua shida ilikuwa ni nini, kasema, “Waangalieni hao ndege, kwa makundi, wakiondoka kwenye kuta, wakienda zao. Hawatatua pale usiku, hawarudi, wanaondoka wala hawarudi. Kondoo hata hawatazikaribia

hizo nyua, wanasimama huko nje wameegemeana wao kwa wao, na ng'ombe." Ndipo tetemeko la ardhi likaja na kuziporomosha kuta hizo. Ndipo hao ndege wakarudi, ilikuwa ni ishara kwamba tetemeko la ardhi lilikuwa limekwisha.

122 Ndugu, Mungu yeye yule ambaye angeweza kuwaongoza kondoo, na ndege kwenye safina katika siku za maangamizi yaliyotangulia ile gharika, ndiye Mungu yeye yule, leo, Ambaye angeweza (na kama Mungu anaweza kusema na ndege aitoroke hatari), "Ondokeni kwenye kuta hizi kubwa za Babeli za kutokuamini, wakati wa kutikiswa unakuja." Roho Mtakatifu akionyesha ishara na maajabu ya maangamizi yanayokaribia.

123 Angalieni, inaweza kutukia wakati wowote, hakuna kitu kimoja kilichosalia, kuja kwa Bwana kumekaribia. Tunaona katika vibanda vya Urusi na ulimwengu wote mbalimbali, mabomu na kadhalika ambayo yangeuangamiza ulimwengu mzima kwa ghafla. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.] Ulimwengu usingeweza kustahimili. Na kabla hilo halijatukia, Kanisa linaenda Utukufuni. Kumbukeni, kabla mvua yoyote haijapata kunyesha, Nuhu alikuwa ndani ya safina, usalama; kabla ya Moto wowote kushuka, Malaika alimwambia Lutu hivi: "Ondoka hapa, toka hapa, maana siwezi kufanya lolote, mpaka umeondoka hapa, uondoke hapa."

124 Kanisa litatoka kabla hayo maangamizi hayajaja, nao ulimwengu wa kisayansi unasema ni dakika tatu ifike usiku wa manane. Saa imesonga wakati wote, Umilele unakaribia kuingia. Ulimwengu unajua, ulimwengu wa kisayansi unajua, ya kwamba, ulisema ingewaogopesha watu hata kufa, mmesikia ninii yao . . . kama wangeyatangaza kwenye redio, na kadhalika. Tunajua wakati umekaribia. Na kama lingeweza kutukia kabla ya asubuhi, na kuondoka kwa Kanisa kunafanyika kabla ya jambo hilo kutukia, kuja kwa Kristo kumekaribia jinsi gani? Amina. Haleluya!

125 Ndugu, nakwambia, huwezi kuchimba chini vya kutosha kujificha kutoka kwa moja ya hayo mabomu, watalipua shimo ardhini kwa maili mia moja na hamsini, kina cha futi mia mbili. Utaingiaje huko chini? Ukijenga ngome ya chuma au jengo la kina cha futi mia tano, huo mtikiso ungevunja kila mfupa mwilini mwako. Imefikia mahali ambapo, hakuna mahali pa kujificha hapa chini, ungeweza kuililia miamba, lakini ninakwambia, kuna kimbilio la kudumu la kuepukia bomu, limetengenezwa kwa manyoya: chini ya mbawa Zake. Amina. Hilo ndilo kimbilio, vivuli vya milele vya upendo na utukufu Wake. Hapo ndipo mahali pa kimbilio, mahali pa kukimbilia.

126 Niliketi milimani wakati fulani uliopita, nikimwangalia maskini mama tai akiwaleta watoto wake kutoka kwenye kiota. Akawaweka chini, walikuwa wametoka kwenye maskini matapiko . . . Samahani tamshi hilo. Kiota cha kale kinanuka,

kama ukiwahi kuwa karibu na kiota cha tai. Ndipo—ndipo akawaweka huko nje. Nami nilikuwa nimeketi, nikichunga ng'ombe, nami nilikuwa . . .

127 Ni wakati nilipokuwa kwenye miamsho hii, lakini nilienda kule kuwaleta ng'ombe kwenye majira ya kuchipua, nami nilikuwa nikiangalia kwa darubini. Na kama nimewahi kuona mkutano wa Kipentekoste, ulikuwa ni wa hao tai wadogo. Hawakuwa wamewahi kuikanyaga nyasi hiyo hapo awali, mwajua, hakuna chochote ila kiota hicho cha kale kinachonata, kinachovunda, kama ulimwengu. Ndipo huyo mama akatandaza mbawa zake kubwa, na kuwachukua, na kuwashusha, na kuwaweka chini katika eneo la Kipentekoste. Walikuwa wakirukiana tu, na hisia hiyo nzuri miguuni mwao, mwajua. Wajua jinsi unavyojisikia unapokuwa na Roho Mtakatifu, ni kama kwamba tu unatembea juu ya manyoya, ama springi, mahali fulani, ukijisikia vizuri tu.

128 Walikuwa na yubile kubwa mno ya Kipentekoste. Ndipo maskini mama huyo, mara alipowaacha, aliruka, akachukua mabawa yake makubwa, akaruka juu ya mwamba mkubwa, mrefu, akakunja mabawa hayo makubwa, akaketi pale na kuangalia nje.

Nikawaza, "Loo, jamani!"

129 Hivyo ndivyo alivyofanya, wakati aliponitoa kwenye kiota cha kale cha ulimwengu, alipanda kwenye maeneo ya Utukufuni, "Na jicho Lake liko kwenye shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia," Yeye anakuangalia.

130 Acha mbwa mwitu aje akitaka, angempeleka juu sana hewani, na kumwangusha, angevunjika-vunjika. Naam, bwana. Hakuna kitu kitakachowadhuru makinda wake, yeye anaangalia hilo.

131 Mungu huliangalia Neno Lake, Yeye huwaangalia watu Wake. Anataka kumpata mtu atakayemwamini, na kumtumainia Yeye aketiye katika utukufu wa juu, akiangalia.

132 Muda si muda mwajua, nikasikia mngurumo, na kijani kutoka hapa kuelekea Washington, hiyo ilikuwa huko Colorado, nikaona mkondo wa kijani ukija, nikajua dho—dhoruba ilikuwa inakuja, ngurumo na radi. Maskini mama huyo akaketi pale, naye akanusa hiyo dhoruba kidogo, kisha akarusha hayo mabawa makubwa, na kupiga mayowe makubwa mno, naye akashuka bondeni. Aliposhuka kwenda kule, alipanua mabawa yake makubwa, akatoa tu mlio mkubwa, na kila mmoja wa hao tai wadogo akakimbia na kuruka moja kwa moja kwenye bawa la mama huyo, kisha wakachukua miguu yao midogo, na kuyashika manyoya, wakaweka mdomo wao mdogo, na kuyashika, ndipo hayo mabawa makubwa mno yakaanza kusogea. Loo, loo, loo, loo! Utukufu! Mtaniita mtakatifu anayejibingirisha, kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali muanze. Naam, bwana.

133 Alipoyachukua hayo mabawa makubwa, alianza kuinuka, moja kwa moja akiukabili upepo huo. Nao wangeweza kuupenya huo upepo ukija maili sitini kwa saa, nao hao tai wadogo wakishikilia bawa hilo, akaingia moja kwa moja kwenye hilo shimo kwenye mwamba.

134 Nikasema, "Ee Mungu!" Nikatupa darubini hiyo chini, na kucheza juu ya hicho kilele cha kilima. Nikasema, "Siku moja nguvu za Mungu zitatandaza mbawa Zake kuu kote duniani, nao tai Wake wataushika huo Mwamba wa Miaka, "Uliopasuliwa kwa ajili yangu, jalia nijifiche Kwako, wakati maji membamba yakitiririka." Naam, bwana. Shikilia kwenye huo Mwamba wa Miaka.

135 Nilikuwa huko Gary, Indiana, nikiwa na mkutano, hapo ndipo maskini msichana huyu, mcheza dansi wa Fred Astaire alipoitwa mkutanoni, na—na Rosella Griffith, yule mlevi sugu, na mambo hayo yote makuu yakitukia hivi majuzi tu. Walinipeleka kwenye viwanda vya chuma kule ku—kunionyesha kote, yale yaliyokuwa, yale waliyokuwa wakifanya. Na mmoja wa hao jamaa, Mkristo, walikuwa na lundo la vikerezo ambapo walikuwa wakiendesha kitu hiki cha duka la mitambo, wakikwangua vitu hivi vyote walivyokuwa wakitengeneza, na kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, filimbi ndogo ikapigwa, na walipofanya hivyo, kila mtu alivua aproni yake, akachukua ufagio wake na kufagia vi—vipande vyote katikati ya sakafu, akasema, "Sasa angalia, Bw. Branham, nitakuonyesha jambo fulani."

Nikasema, "Naam, bwana."

136 Filimbi nyingine ndogo ikapigwa, kila mtu akaondoka. Na chini kupitia chumbani, kwenye hayo marefu kulikuwa kumewekwa lundo kubwa la hivyo vipande, akaenda pale na kubonyeza mlango namna *hiyo*, ama, kitufe namna *hiyo* mlangoni, akakibonyeza, na hii hapa sumaku kubwa mno ikaja, ikinguruma, "*Nguruma*!" ikipiga kelele ikipita, ikishuka kupitia mahali pengine, kupitia mahali pengine, ikishuka, ndipo ikapitia moja kwa moja kwenye vipande hivyo vyote, navyo vipande hivyo vyote vikaruka moja kwa moja juu, kwa sababu vilitiwa sumaku na sumaku hiyo. Akarudi moja kwa moja juu ya kuba kubwa, akavuta kitu kidogo, akaiondoa hiyo sumaku, nayo yote ikaangushwa kwenye tanuru kubwa la kuba ipate kufinyangwa na kufanywa upya.

Nikasema, "Je, hivyo ndivyo mnavyofanya?"

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Haleluya!"

Akasema, "Una shida gani?"

Nikasema, "Sikiliza, niliona hivyo vipande vyote havikuenda. Kwa nini vyote havikuenda?"

Akasema, "Kwa sababu hivyo ni alumini, kwa hiyo havijatiwa sumaku."

"Loo." Nikasema, "Utukufu!" Nikasema, "Kwa nini kipande hicho cha chuma hakikuenda, *pale*?"

Kasema, "Unaona, kimefungwa chini."

Nikasema, "Ee Mungu!"

Kasema, "Una shida gani?"

137 Nikasema, "Ninawazia kuhusu Sumaku nyingine kuu. Haleluya! Mwana wa Mungu akining'inia kule Utukufuni. Siku moja, kutakuwako na sauti kama ya upepo unaoenda kasi, na huyu hapa Yeye atakuja, na wale wote waliotiwa sumaku na Roho Wake watapaa juu kumlaki hewani. Wale waliofungwa pingu za dhambi, wale ambao ni washiriki alumini wa kanisa hawatafanikiwa kamwe. Nasi tutafinyangwa tuwe katika sura ya wana na binti za Mungu."

138 Loo, jamani, itakuwa ni siku ya jinsi gani! Idumishe nafsi yangu imetiwa sumaku, Bwana, kwa Roho Wako zaidi ya vitu vyote. Hebu niende na ufunguo wakati nikipanda ngazi hii. Naam, bwana. Kwa kuwa siku moja Yeye atakuja, Biblia inasema atakuja, nami ninataka nafsi yangu ipatane Naye. Ninataka mkataba huu, kama nilivyouvunja jana usiku, ninataka kujazwa na sehemu *hii* ya mkataba nikingojea *ile* ije, amina, loo, pamoja na agano kama Yeye alivyolithibitisha kwa Ibrahimu.

139 Sasa, Yeye alisema mambo hayo yangetukia. Ninawatakeni mninii. . .Ninataka kuwapa baadhi yetu wazee ujasiri sasa hivi. Ninataka kuninii. . .Huenda mkatofautiana kidogo juu ya jambo hili, kama mkitofautiana, fanyeni hivi tu jinsi, sasa, nifanyavyo wakati ninapokula sambusa ya cheri, hiyo ndiyo sambusa ninayopenda sana, basi ninapokula sambusa ya cheri, ninapouma mbegu siili hiyo mbegu, ninaitupilia tu hiyo mbegu mbali na kuendelea, ninakula hiyo sambusa. Kwa hiyo, ninapokula kuku, wahubiri wote wanapenda kuku, ninapouma mfupa, sisemi, "Kuku huyo hafai kitu," na kumsukuma nyuma, ninakula tu nyama zote kutoka kwenye huo mfupa, na kuuacha mfupa. Kwa hiyo hivyo ndivyo unavyofanya na yale wewe. . . yale nitakayosema sasa. Kama huwezi, kula tu nyama iliyo juu yake, iliyobaki inaonekana kama mfupa, ama—ama mbegu, iache tu, unaona, acha ibaki hapo.

140 Kwa nini usiangalie yale Mungu aliyowafanyia Ibrahimu na Sara? Alionyesha, kwa Ibrahimu na Sara, ninii, hao watoto wawili, yale atakayowafanyia watoto wao wote. Angalieni, mnajua kile alichowafanyia Sara na Ibrahimu? Aliwageuza wakawa kijana mwanamume na mwanamke, hakika aliwageuza. Sasa kumbukeni. . .

Mnasema, "Je, unaweza kuthibitisha hilo kwa Biblia?"

141 Naam, bwana. Sasa, katika kusoma Biblia, unaona, Biblia ni Hadithi ya upendo, Mungu akiwaandikia watoto Wake. Unaamini hilo? Sasa, ninampenda mke wangu, kweli tuna mapenzi ya—ya—ya kweli, mimi na yeye. Kwa hiyo ninapoenda ng'ambo. . .Hiyo ndiyo sababu ninaamini katika neema ya Mungu. Ni—nilienda. . .Tukienda ng'ambo, si—siji na kusema, "Bibi Branham, hebu nikwambie jambo fulani: Usiwe na waume wengine."

Angesema, "Naam, na, kijana mwanamume wangu, usiwe na wake wengine tena, pia." Unaona?

142 Sasa, hayo si yangekuwa ni makazi? La. Tunainama na kuomba mmoja na mwingine. Ninasema, "Mungu akubariki, Mpenzi."

"Nitakuwa nikikuombea, Billy."

143 "Nita—nitakuona tena, Kipenzi." Huyo naenda ng'ambo. Mnaona? Hakuna lingine. Kamwe sitawahi kuishi bila uaminifu kwake, yeye hatavunja uaminifu kwangu, maadamu tunapendana. Mnaona? Unapompenda Mungu, hutamwudhi, hivyo tu, utafanya kila uwezalo. Kwa hiyo hilo ndilo jambo muhimu maishani ni upendo wa Mungu, "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za Malaika wala sina upendo, si kitu mimi," mnaona. Sasa, hiyo ni kweli. Kumbukeni hilo. Upendo. . .

144 Baadaye juma hili, ninataka kuwapa matukio fulani. Kile ambacho kimeshinda mambo, kimekuwa ni upendo. Kinachowashinda wagonjwa, ni upendo. "Mungu aliupenda ulimwengu jinsi hii." Mungu ni upendo, nao wapendao ni wa Mungu.

145 Sasa, huo ni. . .Sasa kumbukeni, huo si upendo wa fileo, huo ni upendo wa Agapao, labda mnajua. U—upendo wa kiungu, si huu hapa "upendo huru," wanavyouita makanisani na mambo kama hayo, bali huu ni upendo wa Agapao, upendo uliotumwa na Mungu, upendo halisi, wa kweli.

146 Sasa, kisha nikienda ng'ambo, nisingemwambia mke wangu jambo hilo. Vema, tunapendana tu, ninaendelea.

147 Sasa angalieni, katika kusoma Bi—Biblia, ni Barua ya upendo kwa Kanisa. Sasa, ninapoenda ng'ambo, Meda huniandikia barua, naye anasema, "Mpenzi Billy, nimeketi hapa usiku wa leo, ndiyo kwanza nimlaze mtoto kitandani," na kadhalika, anasema jambo fulani hapa, lakini mnaona, ni—ninaweza kujua anachozungumzia, maana ninampenda sana, ninajua yote kumhusu, nami ninaweza kusoma katikati ya mistari, najua anachosema, mnaona, nikisoma katikati ya mistari.

148 Sasa, Mungu ameandika Biblia, Waraka wa upendo kwa Kanisa Lake. Mpaka utakaposoma ninii, kwa upendo, kamwe

hutaweza kupitia mpango baridi wa elimu, kumwona Mungu kamwe. Huna budi kuwa na upendo wa Mungu moyoni mwako, ndipo unasoma katikati ya mistari, hapo ndipo kitu halisi kilipo.

149 Nitathamini yale Meda asemayo, bali upendo ninaopata katikati ya mistari ndio unaojalisha kwangu. Hivyo ndivyo ilivyo na Biblia, mimi husoma katikati ya mistari yale Yeye anayosema.

150 Sasa, hebu na tusome katikati ya mistari kwa dakika moja tu: Sara na Ibrahimu wote wawili walikuwa wazee, sasa, kwa hiyo hili litawatoa kwenye mawazo yenu, ama kuua hilo kwanza kabisa Biblia ilisema, mlango ule ule, ya kwamba wote wawili walikuwa na umri mkubwa. Alikuwa na umri wa miaka mia moja, tisini na tisa, naye mkewe alikuwa na tisini, miaka mia moja na miaka tisini.

151 Sasa, tunajua ya kwamba mtu mwenye umri mkubwa, mwenye umri wa miaka mia moja, ameinama mabegani mwake, na—na nywele zenye mvi zikining'inia chini, ndevu zenye mvi, Sarah, maskini nyanya na fimbo yake, kofia ndogo ya mavumbi, mwajua, akienda kote, ndi—ndipo Mungu akamwambia ya kwamba yeye, ni mtoto mchanga tu bado.

152 Kwa hiyo, nawatakeni mwone yale aliyowafanyia, sasa, Yeye aliwageuza wakawa kijana mwanamume na mwanamke. Haya hapa aliyofanya, sasa, kama mtaangalia, mara baada ya yule Malaika kuwatokea, mnaona, sasa huyo, mara baada ya Malaika huyo kuonekana, kubadilishwa kwa—kwao, walirudi wakawa kijana mwanamume na mwanamke baada ya hapo. Sasa, wakati Malaika huyu wa Roho Mtakatifu. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Sara na Ibrahimu wakawa kijana mwanamume na mwanamke.

153 Ninaweza tu kumwona Sara akiamka asubuhi moja, akisema, "Ibrahimu, mpenzi! Mbona, nundu hiyo inatoweka mabegani mwako!"

154 "Mbona, Sara, hayo macho marembo, kama ya Malaika, yanarudi; weusi huo uliofifia uliokuwa machoni mwako, wote unatoweka. Na nywele hizo zinakuwa nyeusi tena."

155 Akawarudisha kwenye umri wa miaka ishirini hivi kila mmoja. Nitawaonyesha kama alifanya hivyo au la, sasa nyinyi angalieni tu, mnaona. Sasa, walifanya safari ya—ya maili mia tatu, hiyo ni safari ndefu sana kwa mzee wa miaka mia moja na mwanamke. Hiyo si ni kweli? Safari ya maili mia tatu kushuka kwenda Gerari katika nchi ya Wafilisti. Ipime kwenye ramani ni umbali gani, uone, ni mbali sana huko chini.

156 Halafu basi jambo ni kwamba, kulikuwako na mfalme kijana kule chini, jina lake Abimeleki, akijitafutia mpenzi naye akampenda Sara, nyanya. Kukiweko na hao wasichana wote warembo wa Kifilisti, waliokuwa kule chini, hao wasichana wa Mataifa, lakini huyu hapa Sara anakuja, akasema, "Huyo ndiye nimemngojea!" Nyanya.

157 Ndipo Ibrahimu akasema, “Sara, una sura nzuri, kwa hiyo nakuomba, sema tu wewe ni dada yangu.” Mnaona?

158 Loo, jamani! Hivi hamwoni yale aliyofanya? Vema angalieni, hata baada ya hayo, Ibrahimu baada ya, hata kufa kwa Sara miaka arobaini na mitano baadaye, Mungu alimjalia kuoa mwanamke mwingine, naye akapata wana saba, mbali na binti. Amina. Mnaona katikati ya mistari, kile alichofanya?

159 Sasa, sikilizeni jambo lingine, kabla Sara hajampata mtoto huyo mchanga, samahani, dada zangu, usemi huu fidhuli, lakini sina budi kuusema, sasa, tunajua ya kwamba ilimbidi Mungu kufanya jambo fulani, hakuwa amerutubishwa, tunajua hilo, Sara alikuwa tasa, asingeweza kupata mtoto, maana alikuwa ameishi naye miaka hii yote, wala hakuwa na mtoto. Sasa, ilimbidi Mungu kulirutubisha tumbo lake la uzazi, jambo la kwanza. Sasa, hawakuwa na chupa hizi za afya na usafi siku hizo, kwa hiyo ilimbidi kumpa tezi mpya za maziwa, kwa sababu kwenye umri huo mishipa hiyo ya maziwa imekauka. Vema, mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja akiingia katika utungu wa kuzaa, angeshikwa na mshtuko wa moyo, ilimbidi Yeye kumfanyia moyo mpya. Kwa hiyo mnaona, Yeye hakumkarabati tu, alimfanya tu msichana mrembo, kama ahadi kwamba atamfanyia kila mwana wa Ibrahimu. Amina.

160 Abimeleki akampenda, nyanya mkongwe, kofia ndogo kichwani mwake, mwajua, na kusema, “Loo, unaonekana mrembo kweli, mpenzi. Unapendeza.” Naam.

161 Upuuzi, Yeye alimfanya msichana mrembo, hakika, alimfanya, kile atakachotufanyia sisi wazee moja ya siku hizi. Atubadilishe tena! Haleluya! “Siku zote za wakati wangu wote,” alisema Ayubu, “nitangoja, hata wakati wangu utakapokuja,” amina, “wakati badiliko langu litakapokuja.”

162 Naam, bwana, tutabadilishwa katika dakika moja na kufumba na kufumbua jicho, na kunyakuliwa pamoja na hao waliofufuka kumlaki Bwana hewani, na kuwa pamoja Naye milele. Loo, nina furaha sana ninaweza kusema mimi ni mmoja wao! Amina. Amina. Ninajisikia kubarikiwa sana, jamani, kuwazia hilo. Haidhuru ni jambo gani linalotukia humu duniani, hilo halina uhusiano wowote nalo, nitaruka moja ya asubuhi hizi.

163 Naam, bwana. Akawabadilisha wakawa. . .Nami nawatakeni mwone jambo lingine, jinsi Mungu anavyowashughulikia watu Wake. Mliona? Sasa, Abimeleki akasema, “Loo, huyo ndiye tu nimekuwa nikimngojea miaka hii yote!”

164 Kwa hiyo, akaenda kumchukua Sara awe mke wake, bali kumbukeni, kutoka kwenye ukoo huo safi ilibidi aje Masihi, basi Mungu akaipiga nyumba yake. Na huyo hapo Ibrahimu

ameketi huko nje, kwa namna fulani tu. . . alikuwa katika ile ahadi. Alikuwa na ninii . . .

165 Sasa, kama huyu angekuwa ni wewe, ungesema, “Sistahili hilo.”

166 Unafikiri Ibrahimu alistahili hilo? La, bwana, baada ya mtu kushuka kwenda kule na kusema hayo kuhusu mkewe, akasema alikuwa ni dada yake, na kumwacha mwanamume mwingine amchukue mkewe apate kujiokoa? Hakika, yeye hakustahili hilo, bali Mungu hakuangalii wewe, kama unastahili ama hustahili, ni imani yako katika yale uliyomwahidi utakuwa, kama tu atakufanyia jambo fulani.

167 Hapo Abimeleki, nadhani ni ndugu mwema, akasali sala zake, akaoga, kisha akanyosha miguu yake mikubwa apate usingizi mzuri, mzuri sana, akakunja mikono yake, na kusema, “Kesho nitamwoa huyu mwanamke mrembo wa Kiebrania.” Akampeleka nyumbani, na—na kumvika nguo za kifahari za kila namna na hereni, na kumpamba kabisa, mwajua. Akiwa na umri wa miaka mia moja tu, mwajua, alikuwa na umri kama huo, lakini—lakini alikuwa amerudi kuwa msichana.

168 Ndipo kesho yake wakati alipowazia angeoa, Mungu alimtokea, ndoto, na kusema, “Wewe ni sawa tu na mtu aliyekufa.” Naam, bwana. “Wewe ni sawa na mtu aliyekufa,” kasema, “umemchukua mke wa mtu mwingine.” Kwa hiyo hilo ni somo zuri, ndugu. “Umemchukua mke wa mtu mwingine.”

169 Vema, akasema, “Mbona, Bwana, Wewe wajua unyofu wa moyo wangu, unajua ya kwamba aliniambia ya kwamba huyo alikuwa ni ndugu yake, naye akaniambia, ‘Huyo ni dada yangu.’ Katika unyofu wa moyo wangu . . . ”

170 Akasema, “Hiyo ndiyo sababu nilikuzuia usinitende dhambi. Lakini mume wake ni nabii Wangu, sitasikia maombi yako, bali mrudishie mke wake, acha akuombee, nami nitakuponya.” Amina.

171 Loo, ninapenda hilo! Neema ya Mungu kwa watoto Wake! Nguvu za imani, nguvu za maombi hubadilisha mambo. Loo, ndugu, dada, tunaishi katika vivuli vya haki Yake, vivuli vya kuja Kwake. Mungu yeye yule aliyeishi katika siku za Ibrahimu ni Mungu yeye yule, leo, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Kuzimu yote haiwezi kamwe kuvunja moja ya ahadi Zake, Mungu hudumu na ahadi Yake. Hakuna kitu kinachoweza kumbadilisha Yeye. Loo, laiti tungalimwamini Yeye, tutambue tu ya kwamba . . .

172 Enyi watu, ninawaambia, ninyi Wapentekoste mnaona mengi sana, na mumeona mengi maishani mwenu tangu mumekuwa watoto wa Mungu, mumeona mengi sana ya wema, na rehema, na utukufu wa Mungu hata imekuwa ni kitu cha kawaida sana kwenu, ni cha kawaida sana. Ha—ha—hamninii . . . Hilo linawafanya mpoteze imani.

173 Loo, mnafikiri tu kuna watu wengi, labda. . . Mkienda huko Afrika, huko chini Asia, huko chini Australia, baadhi ya hao watu ambao hawajapata kuliona, na hebu baadhi yao wenyeji wa Kiafrika, waone hilo likitukia, utukufu wa Mungu ukishuka namna hiyo, jamani, wanaliamini, atachukua maskini sanamu hiyo na kuivunjia ardhini, na kumkumbatia Yesu Kristo, maana hawajawahi kuliona hapo kabla.

174 Wakati mmoja, kulikuwako na mtu, alikuwa amesoma, kamwe hakuwa ameiona bahari, naye alikuwa amesoma habari za bahari, basi alikuwa anaenda, alikuwa na likizo, alikuwa akishuka kwenda baharini. Na kwa hiyo, akakutana na baharia mzee, baharia, mwajua, akitoka baharini, naye akasema alipokuwa akienda zake, akasema, "Kwani unaenda wapi, mtu wangu mwema?"

175 Akasema, "Loo, ninaenda baharini, sijawahi kuiona." Akasema, "Loo, ninatamani kusikia mlio mkali wa shakwe wanaporuka hewani! Ninataka kuona mawimbi ya chumvi kutoka kusikojulikana yakipanda juu na kufunika, ninataka kusikia harufu ya hayo maji safi ya chumvi." Kasema, "Nimesoma habari zake, nimewazia juu yake, lakini," kasema, "Ninaenda sasa kuiona!"

Huyo baharia mzee akatoa kiko chake kutoka kinywani mwake, na kusema, "Sioni kitu cha kuvutia sana kuihusu," akasema, "Nilizaliwa juu yake miaka sitini iliyopita."

176 Mnaona, Yeye alikuwa ameona mengi sana ya hiyo, hata ikawa ya kawaida. Nafikiri hiyo ndiyo shida yetu sisi Wapentekoste, mnaona utukufu wa Mungu sana, hata unakuwa wa kawaida. Kamwe msiuache uwe kitu cha kawaida. Lazima sikuzote tuustahi, na kuuheshimu, na kuuamini kwa mioyo yetu yote, kwa mioyo yetu yote.

177 Mungu ni mwema. Anatutaka tu—tupate kilicho bora zaidi tulicho nacho. Sisi ni watoto Wake, sisi, Yeye anatutaka tuwe na yaliyo bora kuliko yote yaliyopo, sisi ndio zao Lake lililo bora sana, Naye anatutaka tu—tuwe na yaliyo bora kuliko yote yaliyopo. Mnaamini hilo?

178 Huko chini Louisiana tulikuwa na maskini ndugu mweusi kule chini, ndugu Mpentekoste, naye alikuwa mhubiri mzuri, mzee; nilimpenda sana. Naye kwa namna fulani alikuwa na burudani yangu ya kupenda kuwinda. Na kwa hiyo, yeye siku moja walikuwa na mzee mmoja pale, jina lake lilikuwa Gabriel, bali wa—walimwita Gabe, kwa ufupi tu.

179 Basi maskini Gabe alikuwa ni maskini jamaa mzuri, bali yeye—yeye, tusingeweza kumfanya ajipatanishe na kanisa. Mchungaji angemfanyia yote aliyoweza, bali asingejipatanisha na kanisa. Alikuwa na mke mzuri, mtakatifu, mwanamke mzuri, naye aliomba sikuzote. Naye mchungaji alijaribu kumfanya aje kanisani, bali asingekuja. Alipenda kucheza kamari kidogo, na

kadhalika, na kunywa pombe kidogo, kamwe hangejipatanisha na kanisa.

180 Siku moja, yeye na mchungaji walienda kuwinda, basi wakati, njiani wakija nyumbani. . .Sasa, Gabe alikuwa mmoja wa wapiga shabaha duni sana walioko Louisiana, asingeweza kupiga ndani ya ghala huku milango imefungwa. Kwa hiyo, walitoka kwenda kuwinda siku hiyo, na jioni hiyo wakati wakirudi walikuwa wamelemewa na ndege, na sungura, na kadhalika, wanyama wote, ilikuwa Jumamosi alasiri. Walikuwa wakichechemea kwenye njia ya kale, iliyojulikana, kando ya kilima, ndipo mzee Gabe akaendelea kuangalia juu ya bega lake, akiona machweo ya jua. Akasonga, mbele kidogo, na moja kwa moja kwenye shavu lake kubwa jeusi, machozi yakaanza kutiririka. Mchungaji alikuwa ametangulia huku sungura wamefungiwa juu ya vijiti, na kuning'inia juu ya bunduki yake, na akiendelea namna hiyo. Baada ya kitambo kidogo, mkono mkubwa mno, mweusi ukamgusa begani mwake, akaangalia pande zote.

Akasema, "Mchungaji?"

Akageuka, na kusema, "Naam, Gabe."

Kasema, "Unaona lile jua likitua, huko ng'ambo?"

"Naam."

181 Kasema, "Hilo linatua kwenye mapaji yote mawili ya nyuso zetu." Hmm! Kasema, "Linatua kwenye vipaji vya nyuso zetu sote wawili." Akasema, "Unajua nitakalofanya?" Akasema, "Ninashuka kuja kwenye benchi ya waombolezaji asubuhi." Huko chini kusini, sijui kama mnajua benchi ya waombolezaji ni nini hapa, ni madhabahu. Akasema, "Kisha nitasimama kutoka hapo, ninarudi kwa mke wangu wa thamani, na kuketi. Na baada ya mimi, wewe kunibatiza, *mimi* nitakuwa mshiriki wa kanisa hili, na nitakaa katika kanisa hilo hata mauti yatakaponiweka huru."

182 Mchungaji akaangusha bunduki yake, akamkumbatia maskini Gabe, naye akasema, "Gabe, unajua nina furaha kusikia hivyo." Kasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani, Gabe." Kasema, "Ni mahubiri gani niliyohubiri yaliyokufanya ubadilishe nia yako? Au ni wimbo gani tulioimba kanisani uliokufanya ubadilishe nia yako?"

183 Akasema, "Mchungaji," akasema, "ninathamini kila mahubiri uliyowahi kuhubiri, daima niliyafurahia, kwa sababu unasema kweli." Kasema, "Ninafurahia kila wimbo ninaosikia kwaya ikiimba," kasema, "kwa sababu najua unanena juu ya Mbingu na juu ya Mungu." Lakini kasema, "Haikuwa hayo, Mchungaji," akasema, "unajua, Mchungaji, nisingeweza kupiga risasi chochote, sina shabaha," kisha kasema, "angalia tu nyama ambayo Mungu—ambayo Mungu amenipa." Kasema, "Hakika, hapana shaka ananipenda, la sivyo asingekuwa mwema hivi

kwangu." Akasema, "Kwa sababu ananipenda, nampenda, na tangu leo na kuendelea, mimi ni mtumishi Wake."

184 Ndugu, jambo ndilo hilo. Kama tungeangalia tu kote na kuona jinsi Mungu alivyo mwema kwetu, tuhesabu baraka zetu, basi tungekuwa tayari kuchukua mahali petu kwenye kiti Chake cha enzi.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

185 Kuna mtu hapa angetaka kusema, "Ndugu Branham, ninajua ya kwamba Mungu amekuwa mwema kwangu, wala sijakuwa mwema Kwake. Ni—ningetaka kuinua mkono wangu, niseme ni—ninataka kumtumikia, Na—na—nataka Yeye awe Mwokozi wangu. Nitamwinulia mkono wangu sasa"?

186 Sasa, na—naomba ya kwamba unyofu wa moyo wako utakuwa, utafikia mahali sasa, upako huu wenye utukufu wa Roho Mtakatifu. Sasa, ninyi nyote huenda mkawa Wakristo, hilo sijui mimi, bali Roho Mtakatifu anajua, Yeye yule anayefunua siri za moyo atasema nawe sasa na kukufanya ujue kama wewe ni Mkristo au la. Kama akisema ya kwamba wewe si Mkristo, je, utainua mkono wako, useme, "Mungu unirehemu? Sasa ninataka kumkubali Yesu kama Mwokozi wangu"?

187 Waweza kuinua mkono wako, mahali popote humu jengoni? Mahali popote? Mungu akubariki, ninauona mkono huo. Kunaweza kuwako na mwingine? Mungu ambariki huyu mama hapa. Wengine huko juu kwenye roshani mkono wangu wa kulia, njiani, ungeinua tu mkono wako? "Sasa nataka kumwamini Bwana Yesu Kristo. Amekuwa mwema kwangu, sijakuwa mwema Kwake, Ninapaswa kumtolea maisha yangu."

188 Baadhi yenu ninyi vijana huko juu? Ingebadilisha wakati wako wa maisha, umri huo usiojali wa roki. Hivi hutakuja kumtumikia Bwana Yesu na upate Uzima wa Milele? Hebu niwashawishi, katika Jina la Kristo mpatanishwe na Mungu. Mungu ambariki mtoto huyu hapa nyuma, aliyeinua mkono wake.

189 Roshani mkono wangu wa kushoto, sivyo? Mungu akubariki, mwanangu. Loo, mwingine? Mungu akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki, dada mpendwa. Kuna mwingine, ungetaka tu kumkubali Kristo usiku wa leo kama Mwokozi wako? Sema, "Ninataka kukumbukwa katika maombi, Ndugu Branham, Kristo akiwa ni Mwokozi wangu."

190 Chini kwenye orofa ya chini upande wangu wa kushoto, katika marefu haya hapa, mtu fulani huko inua mkono wako ambaye hujainua? Inua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham."

Marefu ya upande wangu wa kulia, huku upande huu? Mungu abariki. Mungu ambariki huyu. Naam. Mungu ambariki

msichana huyu mdogo. Mungu ambariki mama huyu hapa. Hilo ni zuri.

191 Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na tuombe. Ninyi mlioinua mikono yenu, kumbukeni, huyo alikuwa ni Mungu aliyesema nanyi. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu.” Hiyo inaonyesha Uwepo wa Mungu uko pamoja nanyi.

192 Baba yetu wa Mbinguni, jalia wema Wako, na rehema Zako, tujalie, Bwana, zikae juu ya kusanyiko hili asubuhi ya leo, hasa juu ya wale walioinua mikono yao. Sikumaliza somo langu usiku wa leo, Baba, sikulifikia somo hilo, lakini nilijisikia kiajabu sana kusimama kwa wakati uu huu, nikizungumza juu ya wema Wako, jinsi ambavyo Wewe ulimbadilisha Sara na Ibrahimu. Huenda kukawa na wengi humu ndani, Baba, ambao hawatabadilishwa siku hiyo, kama hivyo ndivyo Baba, jalia wainue mikono yao, si mikono yao tu bali na mioyo yao na kukukubali Wewe kama Mwokozi binafsi sasa hivi, wapate kuingia katika Utukufu wa utukufu Kwako katika ushirika kupitia kwa Damu, na wapatanishwe na Mungu, kwa haki ya Kristo. Tujalie, Bwana.

193 Yasikie maombi ya mtumishi Wako tunapowakabidhi wote Kwako, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Amina.

194 Sasa, kabla tu hatujaanza, na kuomba kuja madhabahuni, nilijisikia kigeni sana kuhusu hilo sasa hivi tu. Siamini waligawa kadi za maombi. La, sikudhani hivyo. Kesho usiku . . . Nilisahau kuwaambia hao wavulana wagawe kadi za maombi, tutazigawa kesho usiku kwa ajili ya wagonjwa, kuwaombea wagonjwa, nitawaomba waje huku, wagawe kadi za maombi. Nilisahau kufanya hivyo alasiri ya leo, nimekuwa na shughuli nyingi, nilikuwa kwenye kiamshakinywa asubuhi ya leo, nami nilikuwa na vyumba vilivyojaa siku nzima, upambanuzi, na kadhalika, ulinidhoofisha tu, nami nikasahau kuja kuleta . . .

195 Hata hivyo, kuna yeyote hapa aliye mgonjwa na mhitaji? Inua mkono wako. Una jambo fulani moyoni mwako, inua tu mkono wako, useme, kwa Mungu tu, useme, “Bwana Mungu, unirehemu, sasa nataka kukubali, ninataka kuukubali uponyaji wangu. Ninataka kumwamini Bwana Yesu.” Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni zuri.

196 (Wasemaje?) Vema. Alisema kulikuwa na kadi chache zilizotolewa, tutazichukua basi kesho usiku pamoja na zingine zote.

197 Ninawataka watu hawa walioinua mikono yao, ninawataka madhabahuni katika dakika moja, bali ninataka kuwaonyesha sababu: sababu ya mimi kusimama upesi, kamwe sikumalizia somo langu ilikuwa ni kwa sababu Roho Mtakatifu aliniambia, “Huu ndio wakati.” Yeye daima yuko sahihi. Mikono minane ama

kumi imeinuliwa hapa usiku wa leo, mnaona, kwamba wanataka kumkubali Kristo.

198 Sasa, kuwajulisha, kwa ajili ya wagonjwa kwamba Yeye pia anajua kulikuwako na wenye dhambi hapa, Yeye anajua kuna wagonjwa hapa. Sasa, ninyi msio na kadi za maombi na mnataka kukumbukwa katika maombi, inua mkono wako, useme, "Mimi ni mgonjwa, ninamhitaji Bwana." Kila mahali jengoni, popote ulipo. Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu tena kwa muda kidogo tu na kuomba.

199 Sasa, Baba wa Mbinguni, Wewe unajua mambo yote. Kwenye mkono wangu wa kushoto kuna ugonjwa, Bwana, juu ya mwenye dhambi huko juu kwenye roshani, upande wa kulia kuna ugonjwa. Wewe ni Mungu, nasi tumesimuliwa wakati uliposhuka, Wewe ulijiumbia tu Mwenyewe mwili. Tumeumbwa kwa elementi kumi na sita, Nawe ulifanya nini? Hao walikuwa ni Malaika wawili waliokuwa pamoja Nawe. Ulinyosha mkono tu na kuchota konzi ya kalisi, potashi, na petroli, na nurulimwengu, na ukapulizia tu pumzi humo, nao ukawa mwili, Wewe ukaishi ndani yake, ukatimiza ahadi Yako, Bwana, ukarudi, mwili ukageuka kuwa mavumbi.

200 Nina furaha sana kwamba ninamfahamu Mungu anayeweza kuniita kutoka katika mavumbi ya nchi, anipulizie tu pumzi ya uhai tena, siku moja, nami nitaishi milele katika mwili, lakini, Bwana, jalia iwe kwa kila mtu hapa. Na wakati miili hii migonjwa ikijitahidi, ikiwa na Roho wa Mungu ndani yake, inahitaji uponyaji Baba, Ninaomba ya kwamba utaruhusu ujumbe huu uthibitishwe usiku wa leo, ya kwamba Wewe ni Mungu, na unawaponya wagonjwa. Utie kiraka mwili huu ili tuweze kukutukuza Wewe. Tujalie, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

201 Sasa kwa uchaji, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, ninataka kuanza na kuona kama Roho Mtakatifu atanivusha moja kwa moja kwenye jengo hili, kupitia hapa nikiweza. Mtu fulani aliye karibu nami, ama chochote kile, omba, popote ulipo. Imani yako itamshinda mtu mwingine yeyote, ikiwa tu una imani nyingi. Omba tu.

202 Ninaitazamia Nuru hiyo ya Mungu. Nuru hiyo, kwangu mimi, sijui inamaanisha nini kwako. . .Kwa kawaida huwa na picha hapa ambayo ninaiweka mbele ya kusanyiko, hapana shaka hao wavulana wamefanya hivyo mkutanoni, kuziinua, ile Nuru, picha ya Malaika wa Bwana.

203 Kumbukeni, ilikuwa ni Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli nyikani. Nguzo iyo hiyo ya Moto ilifanyika mwili. Mnaamini hilo? Hakika. Yesu alisema waliposema, "Wewe ni mtu bado hujapata umri wa miaka hamsini, ulisema umemwona Ibrahimu?" Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO."

204 MIMI NIKO alikuwa ni nani? Ile Nuru, ule Moto uliowaka kichakani. Akasema, “Nimetoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.”

205 Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Mtakatifu Paulo, jina lake lilikuwa Sauli wakati huo, alikuwa akienda zake Dameski, ndipo Nuru kuu ikambwaga chini, Nguzo ile ile ya Moto. Naye akalia, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Naye akasema, “Mimi ni Yesu.”

206 Huyu hapa usiku wa leo amepigwa picha, mara ya kwanza katika, historia yote ulimwenguni. Sayansi haiwezi kusema hakuna Kiumbe cha kimbinguni. Huyu hapa. Wapi? Katika kanisa la Kipentekoste pamoja na Wapentekoste. Je, huyo ni Yeye yule kweli? Angalieni ni kazi za aina gani anazofanya, kama ni Roho Wake, atafanya vile vile alivyowahi kufanya. Ninyi ombeni, gusa upindo wa vazi Lake, uone kama Yeye si Mungu yeye yule. Omba tu, kama yule mwanamke alivyofanya aliyegusa vazi Lake.

Unasema, “Naweza kuja na kukugusa, Ndugu Branham?”

207 Hakusema kama ukinigusa, mimi siye Kuhani Mkuu. Mguse Yeye, ndipo Roho Wake ndani yangu atatumia mikono yangu, kinywa changu, macho yangu, kusema nawe, kama yule mwanamke aliyegusa vazi Lake.

208 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, ninataka kuzungumza na maskini mwanamke mmoja, yeye hupiga miayo kwenye wakati huu tu, ameketi hapa pembeni, akiugua ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Je, una . . .? Unaweza kuinua kichwa chako sasa. Je, una kadi ya maombi? Huna? Huhitaji hata moja, unaona. Unaugua ugonjwa wa moyo, umekuwa nao kwa muda mrefu sana. Ni ugonjwa wa fadhaa wa moyo wako. Hautakusumbua tena sasa, uligusa upindo wa vazi Lake. Ulimgusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

209 Unaona, mwenye dhambi uliyeinua mkono wako, ni Yeye yule, aliyeniambia, “Simama sasa.” Anakuja kwa ajili yako, kama unaweza kuamini.

210 Huyu hapa mwanamume, ameketi moja kwa moja kwenye mkono wangu wa kushoto, ameketi huko chini kabisa, anaugua ugonjwa shingoni mwake, mgongoni mwake, akiomba. Laiti ungeamini, bwana, kwa moyo wako wote! Bw. Christiansen. Simama kwa dakika moja tu, bwana. Sikujui wewe. Hiyo si ni kweli? Sijawahi kukuona maishani mwangu, wala kuzungumza nawe. Kama hiyo ni kweli, utikise mkono wako namna *hii*. Hatufahamiani. Hilo ndilo lililokuwa sahihi hasa. Hilo ndilo jina lako hasa. Hayo, yote aliyosema yalikuwa kweli? Unaamini unapokea ulichoomba? Nenda nyumbani na upate ulichoomba.

211 Kama huyo si Malaika yule yule! Hapa nitageuza mgongo wangu, Malaika wa Bwana yuko katika eneo hilo sasa hivi. Angalieni kama ni Malaika yeye yule.

212 Kuna mwanamke aliyeketi moja kwa moja nyuma ya mwanamume huyo, anamwombea mumewe, kwa kuwa haendi kanisani. Unaamini, dada, ya kwamba ataenda kanisani, kama utaninii. . . Simama kama hiyo ni kweli.

Huo—huo hapo mkono wake. Mnaona?

213 Simama, dada, ili watu waweze kukuona. Hivi hukuwa ukiomba, "Bwana Mungu, saidia. . ." kuhusu mumeo, na kadhalika? Je, hiyo ilikuwa ndiyo shauku ya moyo wako, ulikuwa ukiomba nikuite? Inua mkono wako. Amezidiwa sana wakati huu, amesimama pale. Je, mambo hayo yalikuwa ni kweli, yale yaliyosemwa? Kama ni. . . Jambo ndilo hilo. Vema.

Mnaamini? Mwaminini Mungu.

214 Hapa, angalieni kama ni Malaika yule yule aliyekutana na Ibrahimu. Sio mimi, *hiki* ni chombo tu anachoweza kutumia, wewe ni chombo anachoweza kutumia. Kuwa na imani na uamini.

Hebu tuone, ninaamini imeenda upande ule, hebu twende upande huu, tuone kama Bwana Mungu anaweza kutujalia.

215 Sasa, Bwana, huku macho yangu yamefumbwa, na—naomba ya kwamba Wewe. . . watu watafahamu ya kwamba si—si mtumishi Wako, Bwana, ni thibitisho la Neno Lako. Wenye dhambi wataitwa madhabahuni katika dakika moja, na jalia wajue ya kwamba Mungu yeye yule aliyesema na Ibrahimu, aliyeishi katika mwili wa mwanadamu, namna fulani ya mwili Yeye alioumba. . . Sisi ni mwili ambao Yeye aliumba, na kuahidi kupitia haki ya Mwanawe kwamba tungetakaswa na kupewa vipawa, kwamba Roho Wake angetenda kazi ndani yetu kama alivyofanya kabla ya yale maangamizi ya Sodoma. Jalia iwe, Baba, ninaomba, katika Jina la Yesu.

216 Kuna mtu aliyeketi moja kwa moja nyuma yangu, yeye ni mtu wa makamu, na yeye—yeye anaomba kuhusu hali aliyo nayo, ni kansa, na hiyo kansa iko kwenye—kwenye nyonga, sehemu ya nyuma. Huyo mtu ni *mahututi*. Unaamini, bwana, kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu atakuponya? Bw. Honeycutt, amini kwa moyo wako wote sasa, utaponywa. Mungu akubariki, yote yamekwisha sasa, unaweza kwenda nyumbani.

Unamwamini Bwana? Huo ndio wema Wake. Mungu hujibu maombi.

217 Kuna mwanamke aliyeketi nyuma yangu upande huu mahali fulani, anaugua ugonjwa wa fadhaa. Ninamwona, anasimama mbele ya. . . Naam, ameombewa hapo awali kwenye mstari wangu, mahali fulani. Aliponywa, yeye na mwanawe. Anaugua ugonjwa wa fadhaa sasa. Jina lake ni Bibi Booth. Mwamini

Bwana Yesu Kristo, kuwa na imani, na uponywe, naye Mungu atakufanya mzima.

218 Unaamini? Nilikuwa nikitafuta hizo nywele nyeusi na miwani, na zimegawanywa upande mmoja. Nilikuwa nikitafuta kupitia hapa, wala singeweza kukupata. Nilikuona umesimama mbele yangu hapa, bali singeweza kukupata. Mambo hayo ni kweli? Vema. Umepata uponyaji wako sasa. Hicho kitu kimekuondokea, unaweza kuwa mzima, na uende nyumbani na kufurahia afya njema.

Sasa, hiyo imeenda, ninaamini imepitia kote kuzunguka hili jengo, sivyo, mahali fulani, kuzunguka hili jengo.

219 Sasa, kwako wewe uliyeinua mkono wako, utakuja usimame hapa kwa muda kidogo tu? Hakika, Mungu alinisimamisha katika ujumbe wangu usiku wa leo, kasema, "Fanya wito huo wa madhabahuni."

220 Utakuja sasa? Simama *hapa* kwa muda kidogo tu, tunaposimama na kuimba kwa sekunde moja tu. Njoni moja kwa moja *hapa* chini. "Karibu nimeshawishika, sasa kuamini." Mungu angeweza kufanya nini cha zaidi, kuliko kufanya yale anayofanya sasa? Utakuja hapa?

221 Hawa watu humu jengoni, wanaoketi huko nje, bila kuwajua hata kidogo, kuna nguvu mahali fulani, na wengi wenu ninyi watu labda mmewakosoa Wapentekoste (Njoo, ndugu yangu.), Wapentekoste, wakikosolewa kwa kupaza sauti na kunena kwa lugha, mnaona kile Roho yuyo huyo atakachofanya? Linazidi tu kuwa kubwa zaidi na zaidi, kwa sababu kuja kwa Bwana kunakaribia. Hiyo ni kweli. Saa imekaribia.

222 Je, utasimama na kuja hapa, na kusimama hapa chini mbele yangu, ili niweze kukuombea? Kama atayasikia maombi yangu kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka, kunifanya nijue siri ya moyo, utakuja sasa na kusimama?

223 Hiyo ndiyo njia ya kulifanya, njoni moja kwa moja sasa. Hilo ni zuri. Shukeni mje moja kwa moja kutoka kwenye roshani, tutasimama papa hapa, na kukungojea, ewe rafiki; hili ni muhimu zaidi. Moja kwa moja katikati ya ujumbe wangu, kuanza *Yehova-Yire,* nilikuwa nalo moyoni mwangu kufanya ninii—ninii, hoja, ndipo Roho Mtakatifu akasema, "Simama, simama, sasa hivi. Simama, sasa hivi. Waambie habari za wema Wangu, kisha uwaite." Njoni moja kwa moja sasa.

"Karibu nimeshawishika," sasa kuamini;

Mungu akishawishi.

"Karibu nimeshawishika," Kristo kumpokea;
Inaonekana sasa nafsi fulani ku-. . .

Ati nini? Uondoke? Sasa sikiliza, Roho Mtakatifu.

. . . "Nenda . . .

Je, waweza kumhuzunisha Roho huyo akuondokee? La. Njoo. Njoo moja kwa moja.

> . . . njia Yako;
> Wengine zaidi . . . ”

224 Ninataka kusema jambo fulani, mwanamke kiwete anashuka kuja, mwanamke kijana kwenye kiti cha magurudumu akisukumwa huku, mwanamke wa mwisho alishuka kwenye mstari huo hivi majuzi usiku kwenye kiti cha magurudumu, kesho yake usiku akaponywa akaenda nyumbani akiwa mzima. Hiyo ni kweli. Kumbukeni, kutoka kwenye kiti cha magurudumu. Loo, kwenu ninyi mnaoweza kutembea, na msichana huyu akisukumwa huku chini kwenye kiti cha magurudumu: Hivi hamtakuja?

> “Karibu nimeshawishika,” mavuno yamepita!
> “Karibu nimeshawishika,” . . .

Shukeni kutoka kwenye roshani, sivyo, ninyi msiomjua Bwana, kumjua Yeye kama Mwokozi wenu.

> . . . huja hatimaye!

Mavuno karibu yamepita sasa.

> “Karibu” . . .

Unasema, “Karibu nije.”

> . . . haiwezi kusaidia; “Karibu” ni kushindwa tu!
> Huzuni, huzuni, kilio hicho kichungu: “Karibu—lakini kupotea!”
>
> “Karibu . . . ”

Hiyo ni kweli, dada. Kadiri unavyokaribia, ndivyo unavyozidi kupokea kutoka Kwake.

> . . . mavuno yamepita!

Mama huyo alikuja kote kutoka juu kabisa kwenye roshani akishuka. Hilo ni sadikisho halisi. Ni jambo adimu Marekani kuona imani kama hiyo.

> . . . hatimaye yuaja!
> “Karibu” haliwezi kusaidia; “Karibu” ni kama kushindwa!
> Huzuni, huzuni, kilio hicho kichungu: “Karibu—lakini kupotea!”

225 Hebu wazia tu jinsi itakavyokuwa karibu kwenye siku hiyo wakati unapowazia kwamba umepakosa Mahali hapo. Huenda kabla ya asubuhi, labda unatokwa na damu barabarani katika ajali, ukitetemeka, ukigutuka, ukiruka, daktari aseme, “Yote yamekwisha.” Ulihisi mapigo yako ya moyo yakipanda kwenye mkono wako. “Loo, kwa nini sikuenda?”

Roho Mtakatifu akasema, "Hauko sawa, unajua hauko sawa."

"Lakini sikufanya hivyo, niliona aibu, kwa sababu nilikiri kuwa Mkristo."

226 Ndugu, afadhali ulilete papa hapa, kwa sababu ulimwengu mzima utalijua siku moja. Hebu tuliweke sawa, sasa hivi. Njoo. Hivi hutakuja? Mara nyingine tena, wakati nikiwaomba wafanyakazi wa kibinafsi waambatane nao, na kusimama karibu, na ndugu wahudumu, wakipenda, waje karibu na watu hawa hapa tunapowaongoza kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu katika maombi.

"Karibu nimeshawishika," sasa kuamini;

Karibu nimeshawishika kuamini yale Mungu anayosema katika Neno Lake, akisema katika Roho Wake, akishuka na kuonyesha ishara kwamba Yeye ni Masihi.

. . . sasa kuamini;
Loo, inaonekana sasa mtu fulani kusema, "Nenda, Roho . . .

Je, waweza kumhuzunisha Roho huyo akuondokee?

. . . njia Yako,
Siku inayofaa zaidi, nitakuita Wewe."

227 Huenda kusiwe na siku inayofaa zaidi. Sasa, tuna chumba hapa, ninaamini kimeandaliwa, moja kwa moja huko nyuma. Ninataka kuwaombea hawa, halafu tutawarudisha chumbani, hawa wenye dhambi wanaotubu, ndipo tutawaita wale wanaomhitaji Roho Mtakatifu, kisha sote tutarudi pamoja, nyuma humu chumbani, ndipo tutaliruhusu kusanyiko liondoke, ndipo tunaweza kukaa mpaka itakapokwisha.

228 Sasa, ninyi watu mumekuja hapa mkiwa na imani ya kwamba mnaamini ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, na mnamtaka awe Mwokozi wenu binafsi. Yesu alisema, "Mkinionea aibu, nitawaonea aibu mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu kwenye Siku ile. Lakini kama mtanishuhudia, ama kunitetea, nitawatetea Siku hiyo."

Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

229 Baba wa Mbinguni, mwenye rehema, tunakuletea watu hawa usiku wa leo, juu ya maungamo, wakija kwenye maji ya farakano, wapate kunyunyiziwa kutoka, nafsi ya—yao chafu, wapate kuoshwa katika maji kwa Neno, na kuletwa kwenye kufanywa upya Uzima, wakienda kuingia katika patakatifu sasa, wapate kuingia katika Utukufu wa Shekina. Ninaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nao, na utawasaidia.

230 Samehe kila dhambi, na wanapoingia chumbani kupiga magoti pale kwa ajili ya maombi, ninaomba, Mungu, ya kwamba Roho Mtakatifu atamjaza kila mmoja na Roho Mtakatifu, na

jalia yaje tu mabubujiko makuu, yenye utukufu ya Roho Wake. Fanya wahudumu kutoka kwa watu hawa hapa, fanya watenda kazi na wasaidizi katika kila kanisa, zitie moto nafsi zao, wakijua ya kwamba hawawezi kukaa muda mrefu zaidi saa inakaribia ambapo Mwana wa Mungu atakuja.

231 Jalia wapate kanisa zuri la nyumbani mahali fulani katika makanisa haya ya full Gospel hapa, wabatizwe kwa toba na ondoleo la dhambi zao, wajazwe na Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Yasikie maombi yetu tunapowakabidhi Kwako. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

232 Sasa, wahudumu hapa, watawaongoza moja kwa moja pembeni, ambapo tunakutana nanyi, katika dakika moja tu, moja kwa moja hivi, kila mmoja wenu sasa, papa hapa karibu. Tutakutana nanyi mle ndani, katika muda mfupi tu. Njoni moja kwa moja upande huu, moja kwa moja upande wa kulia, nendeni mkamfuate mhudumu huyu papa *hapa*, ambapo tutakutana tu nanyi tena. Papa hapa nyuma, katika dakika moja tu.

233 [Ndugu fulani anasema, "Ndugu Branham?"—Mh.] Naam, ndugu. ["Nilishangaa tu, nilifikiri, hao ni wale walioinua mikono yao kwa ajili ya maombi."] Ati kwa ajili ya maombi? ["Naam."] Kwa ugonjwa. ["Naam."] La, ni kwa wokovu sasa, ndugu.

Vema. Moja kwa moja upande huu. Wewe. . . Vema. Hiyo ni kweli. Njoni moja kwa moja huku. Ndugu wahudumu, tokeni nje.

234 Sasa, ni wangapi hapa ambao hawajampokea Roho Mtakatifu nao wanataka kumpokea Roho Mtakatifu? Je, mtakuja, wakati tukiimba wakati mmoja? Ni wangapi humu jengoni hawajampokea Roho Mtakatifu? Kama Yesu angekuja usiku wa leo, unajua itakubidi kuwa na Roho Mtakatifu, kwa kuwa, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri," Muhuri wa Mungu.

235 Watu hutofautiana, watu husema kuadhimisha siku, ama kufanya jambo fulani, ama jambo fulani ni muhuri wa Mungu.

236 Hilo si la Kimaandiko, Waefeso 4:30 inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Ni wangapi wanaojua hilo? Neno la Mungu lilisema Muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu.

237 Sasa, halafu alama ya mnyama ni nini? Ni kumkataa Roho Mtakatifu, alama ya ukengeufu. Mnakumbuka, katika siku za kale wakati baragumu, Mwaka wa Yubile ulipofika, na baragumu ikalia, na kila mtumwa alikuwa na haki ya kuwa huru? Lakini kama hakuchagua kuwa huru, alipelekwa hekaluni, nao wakachukua uma na kutoboa tundu sikioni mwake, naye alitiwa alama kwa siku zake zilizosalia.

238 Na ni kitu gani? Kwenye sikio, Mungu anapokuita umpokee Roho Mtakatifu, nawe unamkataa, ndipo Mungu analitia alama

sikio lako mahali ambapo hutataka kulijaribu tena. Unaona? Basi hiyo ndiyo alama ya ukengeufu. Na ndipo Biblia ilisema ya kwamba siku hizi za mwisho kutakuwako na matabaka mawili ya watu, Moja likiwa na Alama ya Mungu, Muhuri wa Mungu, hilo jingine likiwa na alama ya mnyama. Hiyo ni kweli? Sasa, unavaa moja ya alama hizo usiku wa leo. Kama ni swali, liweke jukwaani, nitalifikia somo hilo kwako.

239 Sasa, kama hujampokea Roho Mtakatifu, ndio kwanza ujiunge tu na kanisa, waweza kuja, usimame hapa? Huu ungekuwa ndio usiku ambao wengi wenu, hapana shaka, wangempokea Roho Mtakatifu. Wahudumu wazuri, na watu hapa, wafanyakazi, wote wana utaratibu, kama tu ufunguo wa kazi. Nasi tuko hapa. . .?. . .na hakika Mungu amepata neema machoni pako, hakika, laiti ungeweza tu kupata neema machoni Pake. Njoo sasa, Yeye anakutaka, anataka uje. Wote msio na Roho Mtakatifu, njoni sasa tunapoimba *Karibu Nimeshawishika*.

Vema, dada.

“Karibu nimeshawishika,” sasa kuamini;
“Karibu niameshawishika,” Kristo. . .

240 Sasa, unataka Roho Mtakatifu yeye yule aupambanuaye moyo, yeye yule aliyekuwa katika Biblia akifanya hapa, akifanya kazi zile zile, Yeye yupo hapa kukujaza kama alivyofanya katika Biblia. Utakuja?

. . .anakualika hapa, Malaika wanakaa karibu,
Maombi yanapaa kutoka mioyo yenu inayopendeza sana; Ewe mzururaji, njoo.

241 Hebu niwaimbie ubeti mdogo bila muziki:

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
“Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho wa Mungu, taa zenu zimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

Mataifa yanavunjika,. . .

242 Hebu tuuimbe.

. . .Israeli wanaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
“Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu (ulimwenguni kote) inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho, taa zenu zimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia. (Loo, hivi hamtaki . . .?)

Mataifa yanavunjika . . .

Hiyo ni kweli. Yako wapi mazungumzo yenu ya amani, Mabingwa wenu Wanne, Shirikisho la Mataifa, na kadhalika?

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,

243 Ikawa taifa. Mara ya kwanza katika . . .-na tano, miaka elfu mbili mia tano, ile nyota yenye ncha sita ya Daudi inapepea. "Mtakapoona mtini ukichipusha majani yake."

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri; (Nini kinachotukia?)
Siku za Mataifa zimehesabiwa (Loo, ndugu!), zimekumbwa na hofu;
"Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho, taa zenu zimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

244 Ni kitu gani, rafiki? Wakati tutakapobadilishwa. Ukombozi ni . . . Angalieni ishara. Mungu alisema, "Katika siku za mwisho," Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Malaika wa Bwana duniani, akiishi katika mwili wa binadamu, miongoni mwa watu, akifanya ishara na maajabu. Kila kitu kiko tayari, mataifa, mabomu ya atomiki, loo, mazungumzo ya amani, na kila kitu, kama walivyosema wangefanya, Israeli inaamka, mtini unachipusha majani yake, loo, tuko kwenye mwisho, ewe rafiki.

245 Na, "Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu." Mnajua yale Biblia isemayo kuhusu Mataifa. Loo, jamani! Itakuwaje kwa wale watakaokatiliwa mbali? Kwa hiyo njoo ikiwa huna Roho Mtakatifu. "Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu." Hivi hutakuja usiku wa leo, na kusimama kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu? Tutawaombea hawa, na kuwaongoza waingie chumbani, hapo tunaamini ya kwamba Mungu atajaza na Roho Mtakatifu.

246 Watoto, ninyi watu wa thamani, mliosimama hapa usiku wa leo: "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa."

247 Baba wa Mbinguni, tunaomba maombi ya imani juu ya watu hawa waliosimama hapa ambao wana njaa na kiu, tukiwapa Neno Lako, tukiwaambia ya kwamba Wewe uliahidi wamebarikiwa hata kuona kiu, kwa sababu wanakutaka Wewe, Neno la Mungu lilisema wamebarikiwa. Watu wengi hata hawautaki, basi wamelaaniwa; wale wanaoutaka wamebarikiwa, Nawe ulisema watajazwa. Ninakukumbusha hilo usiku wa leo, Bwana Mungu.

248 Nami ninajua unasikia vilio vya watu Wako, Nawe upo hapa kuwakomboa, na kuwatoa utumwani, na kuwaweka katika uhuru wa Roho Mtakatifu, kwa maana imeandikwa, "Ambaye Mwana amemweka huru yu huru kwelikweli." Ninaomba, Baba, ya kwamba utawapa ubatizo wa Roho Mtakatifu wanapoingia sasa kuupokea. Ninawakabidhi Kwako, kama nyara za Wewe kunisimamisha usiku wa leo katika Ujumbe wangu nipate kufanya wito huu wa madhabahuni. Bwana, ninawakabidhi Kwako uwape Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo.

249 Mnaamini Mungu hujibu maombi yangu? Basi ingieni chumbani, wafuateni hawa wahudumu, baadhi yao hapa, watakaowaongoza moja kwa moja kwenye chumba hiki hapa, humo mtampokea Roho Mtakatifu, ingieni moja kwa moja sasa.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;
"Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

Hebu pamoja:

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho, taa zenu zimetengenezwa na
ni safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

Manabii wa uongo wanadanganya, wanaikana
kweli ya Mungu,

250 Ee Mungu! Tuko kwenye wakati wa mwisho jamani, tuko hapa, tunawasili. Kwa nini akanisimamisha usiku wa leo? Kwa nini akafanya hivyo? Sijui. Msifikiri nimerukwa na akili, najua hasa mahali nilipo. Lakini ninashangaa, "Kwa nini?" Kuna mhubiri anayeingia mle? Kuna kitu? Kuna nini? Je, ni wito wa mwisho wa mtu fulani? Sijui. Ajabu, sielewi. Hiyo ni kweli. Siwezi kulielewa. Nilipokuwa tu nikifikia upeo wa ujumbe wangu, akasimamisha, akasema, "Huu ndio wakati! Huu ndio wakati! Nena kuhusu wema Wangu, na kuita." Nami nilifanya hivyo, hasa kabisa, kusudi watu wajisikie hakika.

251 Je, kila mtu humu ndani ana ubatizo wa Roho Mtakatifu? Inueni mikono yenu. Wote walio nao, inueni mikono yenu. Hilo ni sawa. Mungu awabariki. Hilo ni zuri sana. Vema.

252 Je, bado kuna wagonjwa na wanaoteseka hapa ndani, wakati wakiwa chumbani? Inueni mikono yenu kama unataka kukubali uponyaji wako sasa. Ninaamini Yeye ataponya kila mmoja wenu. Hivi hamwamini? Vema, sasa hebu na tufanye kama tufanyavyo kila usiku, tuwekeane mikono mmoja kwa mwingine. Kama wewe—kama unajisikia . . . Kama wewe ni . . .

253 Kila mtu hapa ndani mliinua mikono yenu walikuwa na Roho Mtakatifu, usingeweza kuwa na Roho Mtakatifu bila kuwa mwaminio. Kama wewe—kama ukisema una Roho Mtakatifu, na kukana nguvu za Mungu, una mfano wa utauwa, huku ukikana nguvu zake, unaona, kwa hiyo wewe si mwana wa Mungu, una roho ya upinga-Kristo. Neno la Mungu litasema, kila wakati, ni kweli, Neno la Mungu.

254 Hivi hamna furaha, usiku wa leo, kwamba ahadi ya Mungu . . .? Angalieni hapa, kwenu ninyi Wapentekoste, Biblia ilisema, "Kama ninyi nyote mkinena kwa lugha, wala hakuna mwenye kufasiri, halafu mtu asiye na elimu aje miongoni mwenu, basi ataanguka chini," (Mungu akubariki, mwanangu.) "ataanguka chini na kuwaambia, na kusema, 'Mbona, nyote mna wazimu!'" Hiyo ni kweli? "Lakini kukiwako na mmoja anayetabiri na kuzifunua siri za mioyo, basi watasema, 'Hakika, Mungu yu pamoja nanyi.'" Hiyo ni kweli? Mnaona kile kilicho Kanisani usiku wa leo? Roho wa Mungu akirudi moja kwa moja ndani, jinsi hasa Mungu alivyosema angefanya.

255 Loo, itakuwa Nuru wakati wa jioni, sivyo jamani? Nuru ni . . . Nina furaha sana kwamba Hiyo ni Nuru, nanyi je?

> Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri,
> Njoo ambapo matone ya umande wa rehema ni maangavu;
> Angaza kote kutuzunguka mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Hebu tuuimbe pamoja:

> Tutatembea Nuruni, Nuru hii nzuri,
> Huja ambapo matone ya umande wa rehema ni maangavu;
> Angaza kote kutuzunguka mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.
>
> Enyi watakatifu wote wa Nuru tangazeni,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu;
> Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Hebu tuinue mikono yetu sasa, na tuuimbe:

> Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri sana,
> Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema ni maangavu;
> Angaza kote kutuzunguka mchana na usiku,

Yesu, Nuru ya ulimwengu.

256 Sasa wekeaneni mikono. "Njoni enyi watakatifu, wa imani mkatangaze, Yesu, Nuru ya ulimwengu." Mmeagizwa, enyi marafiki, kama mwaminio, kuwawekea wagonjwa mikono; Agizo la Mungu la kuhakikisha ya kwamba wao, ahadi ya Mungu, hasa, ni kuhakikisha kwamba wamepona, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

257 Bwana Mungu, nimejaribu kukutii kikamilifu. Ninazibariki leso hizi kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka. Roho Yako iko kote jengoni, juu ya watakatifu wote, kupitia kwa watakatifu, ndani ya watakatifu, Mungu pamoja nanyi, kupitia kwenu, juu yenu, ndani yenu, Mungu yupo hapa, Yeye yupo. Tunafuata, tukitembea katika Nuru, kama vile Yeye alivyo katika Nuru. Tuna ushirika sisi kwa sisi, wakati Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatusafisha na udhalimu wote, inaondoa mashaka yote, na hofu, na mahangaiko mbali nasi, akitupa imani kamilifu na matumaini katika Mungu.

258 Sasa, Shetani, ninakutazamisha jambo fulani, ninakunukulia Neno la Mungu. Yesu Kristo, baada ya kufa Kwake, kuzikwa, na kufufuka, na kushinda kaburi, mauti, na kuzimu, juu ya kila kazi uliyopata kufanya ama kila mamlaka uliyopata kuwa nayo, Yeye alikuvua nguo, wewe si kitu ila mdanganyifu, nawe unafichuliwa usiku baada ya usiku.

259 Huwezi kuwashikilia waaminio hawa tena, wamewekeana mikono, hilo ni Neno la Mungu. Yesu alisema, "Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa, wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya."

260 Toka, Shetani! Ninakuapisha kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu kwamba uondoke kwenye kusanyiko hili la watu hawa!

60-0802 El-Shaddai
Eisenhower High School
Yakima, Washington Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org